





Hormel Foods

Watu wa Kuvutia.
Chakula cha Kuvutia.™

# KANUNI YA MWENENDO WA KIMAADILI WA BIASHARA





## KUFANYA MAMBO YANAYOFAA INAVYOFAA





# JEDWALI LA YALIYOMO


Ujumbe kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu Wetu ........ 1

Uadilifu katika Matendo ........ 2

- Fahamu Kanuni Yetu ya Maadili ........ 2
  - Jinsi ya Kutumia Kanuni Yetu ya Maadili ........ 2
  - Ni Nani Lazima Afuate Kanuni Yetu ya Maadili ........ 2
  - Ondoleo za uwajibikaji na Kutohusishwa ........ 2
- Fahamu ni Nini Kinatarajiwa Kutoka Kwako ........ 3
  - Majukumu Yetu Sote ........ 3
  - Majukumu ya Ziada ya Mameneja ........ 3
  - Uwajibikaji na Nidhamu ........ 4
  - Kufanya Chaguo za Kiuadilifu ........ 4
  - Ongea ........ 5

Kujitolea Kwetu kwa Usalama Kwanza ........ 6

- Kulinda Usalama na Afya ya Memba wa Timu ........ 6
- Kulinda Usalama na Ubora wa Chakula ........ 7
- Kudumisha Desturi Salama za Ushughulikiaji Wanyama ........ 8

Kujitolea Kwetu Kuheshimu Kila Mmoja ........ 9

- Kudhamini Uhusishaji, Uenyeji, Utofauti na Kutendea Haki ........ 9
- Kukuza Mahali pa Kazi penye Heshima ........ 10
- Kulinda Usiri wa Kibinafsi ........ 12

Kukuza Uhudumiaji wa Haki kwa Wateja na Washirika wa Kibiashara ........ 13

- Kulinda Ushindani Huru na wa Haki ........ 13
- Kushirikiana na Washirika wa Tatu wenye Uadilifu ........ 14
- Kukusanya na Kulinda Taarifa ya Mhusika wa Tatu ........ 15
- Kutangaza Bidhaa zetu kwa Uadilifu ........ 15
- Kuepuka Migongano ya Maslahi ........ 16
- Kupeana na Kupokea Zawadi na Hisani ........ 18

Kujitolea Kwetu Kulinda Kampuni Yetu ........ 20

- Kudumisha Uadilifu Wetu wa Kifedha ........ 20
- Kusimamia Vitabu Vyetu na Rekodi ........ 21
- Kuhifadhi Mali Isiyohamishika ya Kampuni ........ 22
- Kulinda Taarifa ya Kisiri ya Kampuni ........ 23
- Kuuza hisa Hisa Kisheria ........ 24
- Kuwasiliana kwa Uangalifu ........ 25

Kujitolea Kwetu kwa Uraia wa Shirika wa Uwajibikaji ........ 26

- Kushiriki katika Biashara za Kiulimwengu ........ 26
- Kukataa Ufisadi na Hongo ........ 27
- Kuzingatia Uwajibikaji wa Kimazingira ........ 29
- Kutetea Haki za Kibinadamu ........ 30
- Kushiriki katika Shughuli za Kisiasa ........ 31
- Kuhudumia Jamii Zetu ........ 32

Muhtasari wa Nyenzo ........ 33

# UJUMBE KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU WETU

## Kwa timu yetu ya watu wenye hamasa,



Hapa Hormel Foods, tuko waangalifu katika kufanya maamuzi mema, kuwatendea watu heshima na kuhakikisha kwamba tumecheza sehemu yetu kuzingatia viwango vya ubora wa juu zaidi ambavyo vimetufanya kufanikiwa kwa miaka 130 na tunazidi kuhesabu bado.

Kuna kujitolea kote katika operesheni zetu ulimwenguni ili daima kufanya kazi kwa kanuni za biashara ya uadilifu na viwango vya ubora. Iwe ni katika kutenda linalofaa hapa ndani kwetu au nusu kote ulimwenguni, tunajulikana kwa uadilifu bila mapatano na kuendea mambo kwa njia isiyo ya kawaida hadi kwa kuwa shirika raia la kipekee.

Kanuni Yetu ya Kimwenendo ni zaidi ya maneno tu. Ni jumla ya hatua tunazochukua kila siku ili kuzingatia sheria zinazotumika, kuendesha kampuni yetu kwa uwajibikaji, kujiendesha kama shirika raia mwema, kulinda watu wetu, bidhaa zetu na taarifa, na kuelekeza jinsi tunavyofanya kazi na wengineo, ikijumuisha washirika wetu, wanaotuuzia bidhaa, wanaotufanyia huduma, wateja na watumiaji bidhaa.

Kufuata Kanuni zetu ni jukumu kuu; ambalo huzingatiwa na timu yetu ya watu 20,000 wenye hamasa.

Kimsingi, inahusu imani. Imani ambayo watu wengine wako nayo kwetu na imani tuliyo nayo kwa kila mmoja. Nina imani kubwa zaidi kwa timu hii kufanya jambo lifaalo kila wakati ili kulindana na Hormel Foods.

Tafadhali chukua muda ili kufahamikiana na Kanuni hizi na kuirejelea mara kwa mara mwaka mzima. Fahamu kanuni na sheria zinazobainisha jinsi tunavyofanya kazi na kuhakikisha kwamba vitendo vyako vya kila siku na maamuzi yanaashiria kwa kujivunia malengo na imani za kitamaduni za Hormel Foods.

Asante kwa yote ufanyayo ili kutusaidia kudumisha na kukuza sifa zetu nzuri kama mojawapo ya makampuni ya chakula yenye umaarufu ulimwenguni.

**Jim Snee**

Mwenyekiti wa Bodi, Rais na Mkurugenzi Mkuu

# U UADILIFU KATIKA MATENDO

## Fahamu Kanuni Yetu ya Maadili

**Karibu kwa *Kanuni yetu ya Biashara ya Uadilifu* ("Kanuni" ile).**

**Jukumu lolote ulilonalo katika Shirika la Hormel Foods na mashirika tanzu yake yote ulimwenguni (yanayorejelewa kwa pamoja kama "Kampuni" katika Kanuni hii), mara moja moja katika kipindi kirefu huenda ukakumbana na maamuzi magumu ya kibiashara. Hizo ndizo nyakati ambapo huenda ukahitaji kuuliza swali au kupata ushauri kuhusu njia bora ya kushughulikia hali hiyo. Kwa bahati nzuri, Kampuni yetu hupeana nyenzo kadhaa ambazo unaweza kugeukia kwa ajili ya mwongozo. Tunayo Kanuni ambayo huweka msingi wa chaguo na hatua za mahali petu pa kazi. Tunaweza pia kutegemea memba wengine wa timu, ikijumuisha viongozi na mameneja, wataalamu wa masuala husika na nyenzo zingine zilizoorodheshwa kwenye Kanuni yetu ili kusaidia kuhusu swali au shaka. Pamoja na sheria zetu, Kanuni hizi hutupatia vyombo na nyenzo ili kutusaidia kutenda mambo yanayofaa katika njia inayofaa.**

## Jinsi ya kutumia Kanuni Yetu

Kanuni yetu imeundwa ili kuwa chombo cha urejeleo kinachofanya muhtasari wa sera, sheria na kanuni ambazo hutumika popote tunapofanya biashara. Pata utulivu unapoitumia. Kanuni hii ina taarifa za daraja la juu kuhusu masuala ya kawaida zaidi yanayohusiana na kazi. Hata hivyo, Kanuni hii haiwezi kusimamia kila hali ambayo itatokea katika mahali pa kazi. Ikiwa unahitaji taarifa za ziada, tumia sheria zenye maelezo zaidi na nyenzo zilizoorodheshwa mwishoni mwa karibu kila mada, au wasiliana na mojawapo ya nyenzo za kampuni zinazosaidia sana zilizotajwa kote na kufanyiwa muhtasari mwishoni mwa Kanuni.

## Je, ni Nani Lazima Afuate Kanuni Yetu

Wafanyakazi wote, maafisa na wakurugenzi wa Kampuni (inayotambulishwa kama "memba wa timu" kwa pamoja katika Kanuni hii) ni lazima wazingatie Kanuni kila mahali tutapofanya biashara. Washirika wa kibiashara wa Hormel Foods ni lazima wafanye vivyo hivyo wanapofanya kazi kwa niaba ya Kampuni.



## Ondoleo za Uwajibikaji na Kutohusishwa

Kampuni hii hufanyia Kanuni hii mapitio ya mara kwa mara na kupendekeza mabadiliko ya kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi wa Hormel Foods ("Bodi"). Katika hali nadra sana, Kampuni inaweza kuamua kwamba inafaa kuondoa uwajibikiaji kwa kipengele cha Kanuni hii. Ondoleo kama hizi za uwajibikaji ni lazima zipatianwe pekee na Bodi na ni lazima zirekodiwe.

### SWALI LA MAISHA HALISI

**S Hii Kanuni mpya inaonekana tofauti sana na Kanuni ile ya awali. Je, tuliibadilisha kwa nini? Je, hii ni kibadala cha Kanuni ya awali? Je, na tukitwaa kampuni ambayo ina kanuni na sheria zake yenyewe?**

A Ndio, Kanuni hii inaonekana tofauti sana. Tulibadilisha muundo wake na tukaongezea maudhui zaidi ili kusasisha Kanuni hii na kuifanya yenye kutumika katika mazingira yetu ya sasa ya bishara. Tulifanya pia mabadiliko na kuongezea vipengele ili kuifanya kuwa rahisi kutumiwa na memba wa timu, ikijumuisha marejeleo kwa sera na nyenzo nyingine muhimu ambazo hupeana maelezo zaidi kuhusu mada. Kanuni hii ni kibadala cha Kanuni yetu ya awali na ndiyo inazingatiwa zaidi ya kanuni zingine au sera ambazo zinatumiwa na Kampuni hii. Iwapo kutawahi kuwa na mzozo kati ya mahitaji ya Kanuni yetu na sheria au tamaduni ya kieneo, pata ushauri wa meneja wako, kiongozi au Idara ya Kisheria kwa mwongozo kwa jambo linalofaa kufanywa.

# Fahamu ni Nini Kinatarajiwa Kwako

## Majukumu Ambayo Sisi Sote Hushiriki

- **Fahamu na ufuate viwango vyetu.** Zingatia sheria, kanuni za uthibiti na viwango vya Kanuni na sheria ambazo zinahusu kazi yako.
- **Heshimu wengine.** Husisha na uunde hisia ya uenyeji, ukithamini utofauti ambao kila mtu huleta. Fanya kazi kama timu.
- **Fikiria kabla ya kutenda.** Jiendeshe kwa njia ya uadilifu, heshima na kitaalamu. Fikiria iwapo kitendo chako kinafikia viwango hivi kabla ya kutekeleza.
- **Timiza matakwa.** Kamilisha kozi zote za mafunzo ya lazima na maadili mengine na uzingatiaji wa matakwa kwa wakati ufaao.
- **Shirikiana unapoombwa.** Kuwa mkweli na mkamilifu unapojibu maswali katika ukaguzi, uchunguzi au ukaguzi.
- **Ongea.** Uliza maswali ikiwa jambo fulani halieleweki. Ripoti ujiendeshaji wowote mbaya na ukiukaji wa Kanuni hii, sera zetu au sheria.
- **Kubali vitendo vyako.** Sisi sote tunawajibika kujenga na kudumisha tamaduni ya maadili katika shirika letu kupitia maamuzi na tabia zetu.


## Majukumu ya Ziada ya Mameneja

- **Kuwa mfano mwema.** Himiza uadilifu, utu na heshima kwa wengineo. Kubali Makosa. Kuwa mwenye kutimiza ahadi zako. Usiwahi kusukuma mtu afanye kitu ambacho wewe mwenyewe huwezi kuwa sawa kukifanya.
- **Kuwa wazi.** Unda mazingira ambayo watu wanahisi kuwa huru ili kutoa maoni, kushiriki maoni yao na kuwa na majadiliano ya wazi. Kuwa mwenye kupatikana ili waweze kuzungumza wazi kwako kuhusu maswali yao na mashaka. Sikiliza.
- **Kuwa mwenye kujituma.** Weka matarajio kwa ajili ya memba wa timu na upatiane maoni kwa umakinifu na kwa wakati ufaao ili kuwahimizia kufanya linalofaa.
- **Kuwa mfanya maamuzi mhusishi.** Wakati hauna hakika jinsi ya kupeana mwongozo au jinsi ya kuchukua hatua kuhusiana na suala la kimaadili, tafuta ushauri wa wenzako kwa maoni yao au tafuta mwelekezo kutoka kwa wataalamu wa suala husika ndani ya Kampuni. Kumbuka – hakuna mtu aliye na majibu yote.
- **Kuwa mwelimishaji.** Zungumza kuhusu Kanuni hizi pamoja na memba na jinsi zinavyotumika kwa kazi yao. Wasaidie memba wa timu na wafanyikazi wowote wa muda, wanakandarasi au wahusika wengine wa tatu unaosimamia ili kuelewa matarajio yako na majukumu yao.
- **Kuwa thabiti.** Kila mara kuwa mwenye kuwajibika na wengine pia kwa majukumu yaliyopatianwa na kujiendesha kwa uadilifu, hata wakati ni kugumu.
- **Kuwa makini.** Ingilia kati na ukomeshe tabia yoyote ambayo ni ya kukosea heshima au inayokiuka zile Kanuni kwa njia yoyote na uripoti suala hilo kwa watu wanaofaa katika eneo lako.
- **Usivumilie ulipizaji kisasi.** Kwamwe usiwahi kulipiza kisasi dhidi ya yeyote. Kila mara wafanye wale wengine kuwajibika iwapo watalipiza kisasi.
- **Kuwa mwenye kuunga mkono Mpango huu.** Kama kiongozi, unaweka sauti na nia kwa mpango wetu wa maadili na uzingatiaji. Ikiwa utauzungumzia kwa hali chanya na kuunga mkono kwa njia amilifu, timu yako huenda ikafanya vivyo hivyo.

## Uwajibikaji na Nidhamu

Wakati Hormel Foods hutegemea uadilifu wa kila mmoja na uzingatiaji wa hiari wa Kanuni hizi, Kampuni inatuchukulia kuwa wenye kuwajibikia mwenendo wetu. Memba wote wa timu wanaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu kulingana na sheria inayotumika wakijiendesha vibaya. Orodha ifuatayo sio yenye kujumuisha wote, lakini ukiukwaji wa hizi ni mifano ya ukiukwaji wa Kanuni zetu na/au sera zetu: kukosa kutoa au kutoa taarifa ya urongo kuhusu ukiukwaji; utelekezaji au kutozingatia kwa kihiari kwa msimamizi au meneja kuhusiana na ukiukaji; na aina yoyote ya ulipizaji kisasi dhidi ya memba wa timu kwa kuripoti mwenendo mbaya au kushirikiana katika uchunguzi.

Hatia za kinidhamu zinaweza kuwekwa, hadi kufikia na ikijumuisha kusimamishwa kazi kwa muda na kufutwa kazi. Mkosaji pia anaweza kuhusishwa na kesi ya madai au uhalifu. Tambua kwamba Kampuni hii inaweza kuwa na haki ya kuweka nidhamu kwa ukiukaji wa Kanuni hizi, hata kama mwenendo wa memba wa timu haupandi na kufikia kiwango cha ukiukaji wa kisheria. Kampuni pia itachukua hatua za kurekebisha ili kusaidia kuzuia ukiukaji zaidi.



## Kufanya Maamuzi ya Adilifu

**Wakati wowote ambapo hauna hakika ya jambo linalofaa kufanywa, jiulize:**

- N L **Je, ni jambo halali?**
- N L **Je, linaambatana na sheria za Kampuni na Kanuni zetu?**
- N L **Je, ni la manufaa ya Kampuni na washika dau wetu?**
- N L **Je, wewe ungekuwa sawa nalo likiripotiwa katika vyombo vya habari?**
- N L **Je, litaunga mkono sifa njema ya uadilifu ya Hormel Foods?**

**Ikiwa jibu lolote ni "la" au "sina uhakika," usilifanye isipokuwa msimamizi wako au nyenzo nyingine iliyoorodheshwa kwenye Kanuni hii ishauri kwamba unaweza kuifanya.**

**INAVYOMAANISHA**

### Nia Njema

Kuripoti kwa *nia njema* inamaanisha unaamini unapeana taarifa kamili na ya kweli, hata kama haijathibitishwa kuwa kweli na uchunguzi. Ikiwa utaripoti uendeshaji mbaya katika nia njema na hauwezi kuthibitishwa, hautakabiliwa na matokeo hasi kwa Kuongea.

# ONGEA

## Je, mbona Niongee?

- Sio tu jukumu la kila memba wa timu Kuongea, ni jambo nzuri pia kutenda. Kuongea huifanya Kampuni kujua masuala yanayohitaji kushughulikiwa ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea. Hali kama hizo zinaweza kuwa mbaya sana kadri zisipotajwa.

## Ni wakati gani ninafaa Kuongea?

- Ikiwa uko na swali au unahitaji mwongozo.
- Ikiwa utapata kujua ukiukwaji wa Kanuni au mwenendo mwingine usio wa uadilifu – hata ikiwa ni kujiendesha vibaya unaodhania tu.
- Ikiwa suala fulani litatokea ambalo linaweza kutishia memba wetu wa timu, washika dau, kampuni au sifa yake.
- **Ikiwa unajua kitu fulani, sema jambo fulani!**

## Je, Nitaongea aje?

Hormel Foods hupeana nyenzo nyingi ambazo unaweza kuchagua kutoka kwazo.

- Wasiliana na msimamizi, meneja mwingine, timu ya Kisheria, Raslimali Watu au Maadili na Uzingatiaji wake.
- Tumia ile tovuti isiyomtambulisha mtu: **https://hormelfoods.ethicspoint.com.**
- Nchini Marekani na Kanada, piga simu ya Dharura ya Maadili na Uzingatiaji: 1-833-672-1232.
  - Inchini Uchina, piga: 400-120-0204
  - Inchini Brazili, piga: 0800-000-0092
  - Nje ya Marekani, Kanada, Uchina na Brazili, piga code ya nchi yako, ambayo inaweza kupatikana katika: **www.business.ATT.com/collateral/access.html.**
  - Utakapopiga msimbo wa nchi yako, utaitishwa nambari ya Dharura ya Marekani. Kisha utaunganishwa kwa Mtaalamu wa Mawasiliano kwa lugha asilia.
- Simu zote zinaweza kupigwa bila kujitambulisha.
- Mawasiliano yote na ripoti zitashughulikiwa kwa usiri kadri iwezekanavyo.

## Vipi kuhusu kulipizwa kisasi ikiwa Nitaongea?

- Kampuni haitavumilia ulipizaji kisasi wa aina yoyote ambao unamlenga mtu fulani kwa kuripoti ujiendeshaji mbaya kwa nia njema au kwa kushirikiana na uchunguzi wa ndani.
- Ikiwa unaamini wewe ni mhanga wa ulipizaji kisasi, piga simu kwa Dharura ya Maadili na Uzingatiaji wake maramoja.

## Na kama Nitaongea kupitia Simu ya Dharura?

- Timu ya Maadili na Uzingatiaji wake au mwakilishi wa Simu ya Dharura ya mhusika wa tatu atatengeneza ripoti ya swali lako au mashaka.
- Nambari za simu na anwani za IP hazifuatiliwi wakati wa kuwasiliana na Simu ya Dharura.
- Taarifa yote itahifadhiwa kwa usiri iwezekanavyo, ikijumuisha utambulisho wako. Ni wahudumu wa Kampuni wanaohitajika pekee watapitia suala hilo na kuamua hatua zinazofuata. Wakati mwingine jina lako huenda likahitaji kushirikiwa, kama vile na mchunguzi; hata hivyo, hatutafahamisha viongozi wako kuhusu ripoti yako. Tunakuhimiza upatiane jina lako kwa kuwa itasaidia kuendesha uchunguzi.
- Uchunguzi utafanywa ikiwa inahitajika. Wewe na wengine huenda mkahojiwa. Ni muhimu kushirikiana na mchunguzi.
- Endelea kufuatilia ili kujua hali ya ripoti yako. Ikiwa uliripoti bila kujitambulisha, uchunguzi huenda ukacheleweshwa ikiwa hautaangalia hali ya ripoti yako. Huenda kukawa na ombi lililochapishwa ambalo linakungoja ili upatiane taarifa zaidi kabla ya uchunguzi kuendelea.
- Ikiwa ripoti yako itadhibitishwa kuwa ya kweli, Kampuni itachukua hatua inayofaa. Utafahamishwa ya kwamba suala lilitatuliwa, lakini matokeo yake huenda yakawekwa kwa siri. Likikosa kuthibitishwa, utafahamishwa pia.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Kutolipiza Kisasi / Kutoadhibiwa

U

# KUJITOLEA KWETU KWA USALAMA KWANZA

**Hakuna kilicho cha muhimu zaidi kwa tulio sisi kama kujitolea kwetu kwa usalama na afya ya watu wetu, ubora wa bidhaa zetu na maslahi ya wanyama walio chini ya uangalizi wetu. Ili kutimiza kujitolea huku, tumechukua baadhi ya viwango vya usalama wa juu zaidi, vya kiafya na usalama wa chakula/ubora katika sekta yetu.**

## Kulinda Usalama na Afya ya Memba wa Timu

Jambo muhimu kwanza kwetu ni kuwa na mazingira salama ya kufanyia kazi kwa memba wa timu yetu na wageni. Tumejitolea kufanya kazi pamoja ili kuondoa hatari na desturi ambazo huchangia majeraha na magonjwa husiani na kazi huku tukishughulikia afya, usalama na hatari za kiusalama katika maeneo yetu ya kazi.

### Tenda Linalofaa

- **Usiwahi sahau - Usalama kwanza.** Ni jukumu lako kujiweka mwenyewe na memba wa timu yako salama kwa kufuata sheria zote za afya na usalama na sera za Kampuni za usalama ambazo ni husiani na kazi yako. Usipuuze mienendo hatari ya wengine ambayo hukiuka sheria zetu za afya na usalama. Saidia wafanyakazi wenza, washirika wa kibiashara, wafanyakazi wa muda, makandarasi na wahusika wengine wa tatu kufuata sera zetu za usalama na michakato.
- **Linda kituo chako.** Usalama wa kuonekana ni sehemu muhimu ya mahali salama pa kazi. Usalama wa kituo hupungua wakati kufuli, kadi za ufunguo na kamera za upelelezi havitumiki vyema.
- **Kuwa makini na mwenye kufaa kufanya kazi.** Usiwahi kufanya kazi ukiwa mwenye kulewa pombe, vitu vilivyodhibitiwa, dawa za kulevya au dawa zinazohitilafiana na uwezo wa kufanya kazi kwa usalama. Ikiwa pombe itapatianwa katika hafla ya Kampuni, kunywa kwa kuwajibika. Usije kazini wakati uko na ugonjwa wa kuambukizanwa.
- **Usiwahi kuvumilia vurugu za kazini.** Hii inajumuisha mwenendo ambao ni wa kutishia, fujo, hamaki au wa kuvurugana, ambao ni lazima uripotiwe kwa usimamizi maramoja. Kwa kuongezea, bunduki na silaha hazikubaliwi popote katika vituo vya Kampuni.
- **Kuwa mwangalifu dhidi ya hatari.** Unacheza nafasi muhimu kwa kuwa na ufahamu wa watu wengine, mazingira ya kuonekana pale kazini na kubainisha hatari za usalama. Ukiona mtu fulani au jambo ambalo linaonekana kuwa kasoro au lisilofaa, ripoti maramoja.
- **Ongea.** Ripoti kwa haraka hali zozote hatari au zisizo salama, majeraha au magonjwa husiani na mahali pa kazi.

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Tulikuwa na visa kadha za wizi katika kituo chetu hivi majuzi, na mwanamke alishikwa peupe kiwandani akiwa na bidhaa zote zilizoibwa – vibeti, vipochi na vipatakalishi. Huwa tunatumia Vitambulisho vyetu ili kuingia katika majengo yetu, kwa hivyo angewezaje kupata kuingia?**

**J** Watu ambao wameazimia kutekeleza wizi, ghasia, hujuma au vitendo vingine hasi mara nyingi hujaribu kufungua lango la kituo kwa kumfuata memba wa timu ambaye ako na beji ya Kitambulisho. Kuwa na hisani, memba wa timu watatelezesha Vitambulisho vyao na kumshikilia mlango mtu afuataye ambaye hana beji. Kumbuka, memba wote wa timu wanaoingia katika vituo vyetu ni lazima watumie beji za Vitambulisho vilivyopatianwa na Kampuni ili kuingia. Wageni na wanakandarasi ni lazima wafuate hatua za Kampuni za kuruhusu michakato ya kuingia kabla ya kuingia. Kufunguliana mlango au kuruhusu uingiaji bila kitambulisho ni ukiukaji wa hatua za usalama za Kampuni na kamwe hairuhusiwi – iwe unamjua mtu huyo au hapana. Huu ni ukiukwaji mbaya wa usalama wa kuonekana. Memba wa timu ni lazima wavae beji zao za Kitambulisho hali wakiwa katika maeneo ya Kampuni. Ukiona mtu kwenye jengo asiye na Kitambulisho kinachofaa, ripoti.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Mahali Pa Kazi Pasipo na Dawa za Kulevya
- Sera ya Usalama wa Umeme
- Sera ya Usalama wa Moto
- Sera ya Uchunguzi wa Majeraha na Ugonjwa
- Sera ya Ugonjwa wa Kutishia Maisha
- Sera ya Majukumu ya Usalama Kiwandani
- Ratiba ya Matakwa ya Usalama
- Sera ya Mahali pa Kazi Pasipo na Tobacco
- Sera ya Majeraha Yanayohusiana na Kazi
- Sera ya Kufunga kwa muda / Kudhibiti Kawi Hatari
- Sera ya Mavazi Maalumu ya Kujikinga Kibinafsi

# Kulinda Usalama na Ubora wa Chakula

Kama kampuni ya chakula inayosifika ulimwenguni, usalama wa chakula ni muhimu sana kwa sifa yetu. Watumia bidhaa na wateja wanaamini Kampuni hii kutengeneza bidhaa salama, za chakula za ubora wa juu. Wale kati yetu ambao hufanya kazi katika uzalishaji wa chakula na michakato ya usambazaji wanawajibika kutekelezesha imani hiyo kwa kufuata kila wakati tamaduni ya utengenezaji mwema wa bidhaa, huhifadhi na usafirishaji. Huwa tunachukua jukumu hili kwa kumaanisha sana na kuweka juhudi za kudumisha imani ya umma katika usalama, ubora na thamani ya bidhaa zetu.

## Tenda Linalofaa

- **Fuata sheria na viwango vyetu vya ubora.** Jitolee kufuata sheria zote za usalama wa chakula na sera za Kampuni zinazohusu kazi yako. Hakikisha kwamba wafanyikazi wenza na washirika wa kibiashara wamefanya hivyo. Kuwa asiyevumilia uzembe au njia mkato katika kushughulikia na kuzalisha bidhaa zetu.
- **Hakikisha rekodi za uzalishaji na ushughulikiaji bidhaa ni sahihi.** Tekeleza ukaguzi wa ubora na uwekaji rekodi, vipimo vya uzalishaji, uhifadhi/hali joto katika usafirishaji na data nyingine ambayo lazima ijazwe na kurekodiwa. Usirekebishe, kugeuza, gushi au kusongeza tarehe ya data. Hakikisha uhifadhi wa nyaraka wa wakati unaofaa na sahihi wa kaguzi zote na ugunduzi.
- **Ongea.** Ripoti maramoja kwa msimamizi wako jambo lolote ambalo linaweza kuathiri usalama na ubora wa bidhaa zetu za chakula.

PATA KUFAHAMU

### HAKIKISHA BIDHAA ZETU ZA CHAKULA NI SALAMA

- **Kaa nyumbani ikiwa uko mgonjwa ugonjwa wa kuambukizana.**
- **Osha mikono na ufuate desturi njema za utengenezaji bidhaa (Good Manufacturing Practices, GMP) za nguo, mavazi ya kujikinga na ushughulikiaji bidhaa.**
- **Dumisha maeneo ya uchakataji safi na bila mchafuko.**
- **Zuia kuenezeana uchafu kati ya bidhaa mbichi na zilizo tayari kula.**
- **Epusha kitu chochote kigeni au uchafu wa kemikali kwenye viungo vya chakula au bidhaa.**
- **Fuata michakato ifaayo ya usafishaji mitambo na matengenezo.**
- **Uzingatiaji wa Matengenezo pamoja na usalama wa chakula na sera za ubora kuhusiana na uzalishaji na uhifadhi wa chakula na bidhaa zilizokamilika kutengenezwa.**

SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Mfanyikazi mwenzangu aliingia kwa chumba cha kupumzika kutoka kwa eneo la uzalishaji wa bidhaa, akanawa mikono yake, kisha akala chakula chake cha mchana. Baada ya kula, alifululiza moja kwa moja kurudi kwa kazi yake ya uzalishaji wa bidhaa bila kusimama anawe mikono yake tena. Je, hili ni tatizo?**

**J** Ndio. Sheria zetu za usafishaji mikono ni kwa misingi ya sheria za usalama na viwango vya ubora. Sera yetu inahitaji memba wa timu ambao wanahusika na kipengele chochote cha utengenezaji wa chakula kunawa mikono yao kabla ya kuguza au kushughulika na kiungo chochote kiingiacho au kiguzanacho na bidhaa ya chakula. Mfanyikazi mwenzako angepaswa kunawa mikono yake kabla ya kurudi kazini. Kama memba wa timu, unapaswa kujulisha mwenzako kufuata mikakati yetu ya ubora na usalama wa chakula inayojumuisha taratibu zinazofaa za usafi. Ni jukumu la kila mmoja kukumbusha wafanyikazi wenzake kufuata itifaki zetu za usalama wa chakula iwapo watasahau.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Wasiliana na timu yako ya usimamizi wa ndani wa kudhibiti ubora au usimamizi wa kudhibiti ubora

# Kudumisha Desturi Salama za Kushughulikia Wanyama

Tumejitolea kudumisha viwango vya ubora wa juu zaidi kwa maslahi ya wanyama kote katika kwenye safu nzima ya usambazaji na mchakato wa uvunaji. Hormel Foods ina sera ya kutovumilia utesaji wa wanyama kupitia kudhulumu au utelekezaji. Mazingira bora na ya utu yatatolewa kwa kila mnyama katika maisha yake, ikijumuisha kupunguza mfadhaiko, kusimamia mahitaji ya kijamii na kudhibiti hali joto.

## Tenda Linalofaa

- **Kumbuka ya kwamba usalama wa mnyama unakutegemea wewe.** Ikiwa unafanya kazi na wanyama au katika eneo ambalo wanyama wamewekwa, fuata sera zote za kampuni za kushughulikia wanyama kwa usalama.
- **Kuwa makini kutafuta dalili zozote za mateso.** Ni jukumu la uadilifu la memba wote kuhakikisha kwamba wanyama wowote wanaopatana nao pale kwenye Kampuni wanatendewa vyema na kwa usalama na memba wote wa timu, wasambazaji bidhaa na washirika wengine wa kibiashara wanaotangamana na wanyama. Ukiona jambo linalokupa mashaka, usilipuuze.
- **Ongea.** Ripoti dhuluma zozote zinazowezekana, utelekezaji au mateso ya wanyama walio chini ya uangalizi wetu, iwe hali yenyewe ni ya kimakusidi au ya kiajali.



PATA KUFAHAMU

### MAMBO MATANO YA DESTURI NZURI ZA MASLAHI YA WANYAMA

**Kwa kila mnyama aliye chini ya ulinzi wetu, tunastahili:**

- **Kuweka mbinu za kufikia maji na lishe bora ili kutimiza mahitaji ya kila siku.**
- **Dhibiti hali ya mazingira ili kupunguza mfadhaiko usiofaa kwa wanyama.**
- **Zuia hali zinazosababisha maumivu au majeraha yanayowezekana kwa mnyama.**
- **Kutoa nafasi ya kutosha, vifaa vinavyofaa na matumizi mazuri ya vifaa vya kuthibiti wanyama.**
- **Punguza au maliza uoga na mfadhaiko unaosababishwa na mwingiano na watu, vifaa au wanyama wengine.**

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S Nilikuwa nimetembelea kiwanda mojawapo ya vile vya wahusika wa tatu vya kuvuna wanyama, ambako niliona zizi la kuzuilia likiwa limejaa nguruwe ambao walikuwa na vidonda vidogo. Wanyama katika zizi zingine hawakuwa na majeraha hayo. Nafikiri zizi hilo huenda lilikuwa na msumari uliojitokeza au kifaa kingine kikali ambacho huenda ndicho kinasababisha haya. Sikufanya jambo lolote wakati huo, lakini wafikiri ningefanya?**

J Ulifanya jambo lililo njema kugundua haya na kuomba mwongozo, hata kama hufanyi kazi katika kiwanda hiki. Wakati huo mwingine, unapaswa kuibua suala hilo kwa ufahamu wa wasimamizi wa eneo la uzuiliaji au kuripoti kwa meneja wa kiwanda.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Kanuni ya Nidhamu ya Msambazaji Bidhaa
- Sera ya Uangalizi wa Wanyama

# KUJITOLEA KWETU KUHESHIMU KILA MMOJA

**Tunapofanya kazi pamoja ili kutendeana mmoja kwa mwingine kwa heshima na haki, na kujenga uhusiano badala ya utengano, tunajenga mahali pa kazi panapokaribisha na pa kitaalamu. Tunawatendea wengine jinsi tungependa kutendewa. Ni rahisi jinsi hiyo.**

## Kuthamini Uhusishaji, Uenyeji, Utofauti na Kutendea Haki

Tunaweka juhudi ili kudumisha tamaduni ya utofauti na uhusishaji ambapo kila mmoja anakuwa na hisia ya uenyeji. Kila mmoja wetu ana haki ya mahali pa kazi ambako tofauti tunazoleta zimekaribishwa na kuthaminiwa. Utofauti kati ya memba wa timu, wateja, wasambazaji bidhaa na washirika wengine wa kibiashara hutusaidia kuhudumia wateja wetu kwa njia bora zaidi. Tunapenda kutendeana kwa haki kwa kuhimiza fursa sawia, kwa sababu kila mmoja anastahili fursa ili aweze kufanikiwa.

### Tenda Linalofaa

- **Tunaunga mkono uhusishaji, uenyeji na utofauti kwa dhati.** Tunatambua na kukaribisha wafanyakazi wenza na washirika wa kibiashara kwa kuwa tayari kusikiza maoni yao, mawazo na tamaduni na kuwa makini kwa masuala ya kijamii ambayo huenda yakawaathiri. Kuunga mkono wafanyikazi wenza kwa kuwa washirika, na kuwahimiza kufikia vikundi vyetu vya nyenzo za wafanyikazi (Employee Resource Groups, ERG).
- **Wasimamizi – Kukuza fursa sawia.** Ajiri, dumisha, pandisha madaraka, fidia na nidhanu kwa misingi ya hitimu za mtu, ujuzi na mafanikio yaliyodhihirishwa au vitendo, na sheria husika – kamwe isiwe kwa misingi ya sifa za mtu zisizohusiana. Kuwa mwangalifu kwa jinsi upendeleaji wako huenda ukaathiri aina hii ya maamuzi.
- **Ongea.** Ibua suala hilo ikiwa umeshuhudia au wewe ni mlengwa wa ubaguzi usiokubalika kisheria au tabia ambayo inawatenga wengine.



PATA KUFAHAMU

### FURSA SAWIA

**Ubaguaji wa watu kwa misingi ya makundi yaliyolindwa ni kinyume cha sheria nchini Marekani na mataifa mengine na inaenda dhidi ya kujitolea kwetu kutenda lililo sawa. Kampuni inapeana uajiri sawia na fursa sawia za kujiinua kwa watu wote waliohitimu na haibagui kwa misingi ya jamii, rangi, dini, jinsia, mwegemeo wa kingono, utambulisho wa jinsia, asili ya kitaifa, umri, ulemavu, hali ya kijeshi au sifa nyingine yoyote inayolindwa na sheria au sera za Kampuni.**

### MANUFAA YA UHUSISHAJI NA UTOFAUTI

**Mazingira karibishi na utofauti huchangia:**

- **Ushirikiano na ubunifu kwenye eneo la kazi.** 
- **Ushirikishaji na ukuaji wa kutaalamu miongoni mwa memba wa timu.** 
- **Wateja anuai na wingi wa wateja wa bidhaa yetu kuu, yenye kusifika.** 
- **Sisi ni nani kama shirika na kama kiongozi katika sekta.** 

## JINSI YA KUWA MHUSISHAJI ZAIDI

- **Kuwa huru kupokea maoni.**
- **Kuwa tayari kusikiliza.**
- **Wafahamu na kuwahusisha wafanyikazi wenza ambao kwa kawaida hawaingiani nawe.**
- **Usidhanie.**
- **Epuka matamshi ya kuhukumu.**
- **Hoji maoni yenye upendeleo na usaidie kuelimisha wengine.**
- **Tumia nomino/majina/maneno ifaavyo.**
- **Kuwa mshirika wa wengine.**



## SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Mfanyikazi mwenza mpya ambaye amehama kutoka Iraq amejiunga na timu hivi karibuni. Tumeambiwa kwamba atakuwa akiendesha dini yake pamoja na kutafakari na kuomba wakati wa vipindi vya mapumziko. Leo nilimuona akiosha miguu yake kwenye sinki ya msalani. Wafanyikazi wenza na mimi tunadhani kwamba huo ni uchafu. Je, desturi hii inaweza kusimamishwa?**

**J** La. Kampuni imejitolea kuvumilia desturi za kidini za memba wa timu kwenye eneo la kazi kuambatana na majukumu ya Kampuni chini ya sheria inayotumika. Kulingana na Baraza la Mahusiano ya Kiuislamu ya Marekani, "Waislamu wanatakiwa kuosha uso wao, mikono na miguu kwa maji safi kabla ya maombi. Kuoga hufanywa kwenye sinki ya msalani au vituo vingine vyenye maji yanayotiririka." Hivyo basi, Kampuni itavumilia desturi hii na kuiruhusu katika viwanda vyetu, lakini huenda ikaweka vizuizi, kama vile kutenga sinki moja itumiwe kwa ajili ya desturi hiyo.

NYENZO

### Ili Kujifunza Mengi Zaidi

Fikia taarifa kuhusu uhusishaji na utofauti kwenye Pivoti chini ya Ukuzaji Talanta.

- Baruapepe: Uhusishaji_na_Utofauti@hormelfoods
- EEO na Kauli ya Fursa kwa Wote
- Sera ya Fursa za Ajira kwa Usawa

## Kukuza Mahali pa Kazi penye Heshima

Sote tuna haki ya kufanya kazi katika mazingira yenye heshima ambayo hayana vitisho, dhuluma na unyanyasaji. Kampuni haivumilii unyanyasaji wowote, ikijumuisha unyanyasaji wa kingono na uonevu, ambao hulenga memba yoyote wa wafanyikazi wetu. Uhuru kutoka kwa unyanyasaji na dhuluma hujenga tamaduni ya heshima na husishi ambapo sote tunaweza kuwa wazalishaji, na kila mmoja anahisi kuwa anaheshimiwa.

**INAVYOMAANISHA**

### Unyanyasaji Kinyume cha Sheria

Unyanyasaji ni wa tabia za kimwili, maneno, usio wa maneno au za kingono ambazo ni kinyume cha sheria wakati itatimiza vigezo hivi:

- Hazitakikani.
- Ni za kuudhi kwa mtu mwenye akili timamu.
- Ni mbaya sana na potovu.
- Inahusiana na au hufanywa kwa sababu za mpangilio unaolindwa kisheria.

Tabia fulani za dhuluma au kutishia huenda zisiwe halali kisheria, lakini tabia yoyote ya aina hii bado ni ukiukaji wa sera za Kampuni.

PATA KUFAHAMU

## MIFANO YA UNYANYASAJI

**Unyanyasaji huja kwa nia tofauti na unaweza kuonekana jinsi hii:**

- **Kusumbuliwa kingono au maombi ya kufanya ngono.**
- **Maoni yasiyohitajika, viashiriaji au kuguzwa kimwili.**
- **Barua za kibinafsi zisizohitajika, arafa, machapisho kwenye mitandao ya kijamii au baruapepe.**
- **Uonyeshaji wa nyenzo za kingono au vingine vinavyoudhu.**
- **Mizaha inayoudhi ya kingono, kikabila au maoni.**
- **Matukano, vitisho au dhihaka.**
- **Kuwaita wanyanyasaji "wahanga" au wahanga "walalamikaji."**

## Tenda Linalofaa

- **Saidia kuunda mazingira ya kazi ya heshima.** Watendee wafanyakazi wenza, washirika wa kibiashara na wateja kwa heshima na kiutaalamu nyakati zote, wakati wa na baada ya saa za kazi, na katika mazingira yote ya kazi, ndani na nje ya mahali pa kazi.
- **Chukua hatua.** Saidianeni kwa kuongea wakati mwenendo wa mtu fulani unakufanya wewe au wengine kukosa faraja. Jaribu kuingilia ikiwa utashuhudia tabia ya kudunisha au unyanyasaji na umwambie mkosaji akome.
- **Ongea.** Usiwahi kuvumilia au kupuuza vitisho au tabia ya unyanyasaji wa aina yoyote. Mwambie meneja au mwakilishi wako wa Raslimali Watu kuhusu mwenendo wowote unaoshuhudia ambao niwa kudunisha, la kashfa, la kudhulumu au kunyanyasa.
- **Mameneja wanawajibika kuchukua hatua.** Wale walio katika nyadhifa za usimamizi wana jukumu maalumu la kushughulikia unyanyasaji wanapofahamu kuuhusu. Ni lazima waingilie kati ili kukomesha tabia hii, kisha waripoti haraka kwa Raslimali Watu na Idara ya Maadili na Uzingatiaji.



## SWALI LA MAISHA HALISI

**S Nilikuwa nikila maamkuli ya mchana pamoja na wafanyakazi wenza jana, mmoja wao alifanya mzaha kumhusu mtu aliye na ulemavu. Kila mmoja pale kwenye meza ile alicheka. Ilikuwa saa za maamkuli ya mchana, na kila mmoja alionekana kufurahia mzaha ule. Yule mwenye kutoa mzaha ana ulemavu huo huo, kwa hivyo ilikuwa sawa kwake kutoa mzaha huo?**

J La. Aina yoyote ya mwenendo ambao humdunisha mtu mwingine haukubaliki popote wakati wowote katika mazingira ya mahali pa kazi katika Kampuni. Haijalishi iwapo yule mtoa mzaha ana ulemavu sawia au ikiwa au iwapo ni muda wa mapumziko. Hata ikiwa wote katika ile meza walicheka, mmoja wao au mtu fulani akiskia kwa mbali huenda angeudhika. Suala kuu ni hili: Kujitolea kwetu kutendeana heshima mmoja kwa mwingine hakuzingatiwi na aina hii ya mwenendo na hakujengi mahali pa kazi panapohusisha kila mtu. Mizaha ya kukashifu au maoni hayana nafasi katika tamaduni yetu.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

Fikia taarifa kuhusu uhusishaji na utofauti kwenye Pivoti chini ya Ukuzaji Talanta.

- Baruapepe: Uhusishaji_na_Utofauti@hormelfoods.com
- Sera ya Unyanyasaji
- Sera ya Tabia Kazini
- Sera ya Kutolipiza Kisasi / Kutoadhibiwa

# Kulinda Usiri wa Kibinafsi

Baadhi yetu tuko na ufikiaji wa taarifa za kibinafsi za wafanyikazi wenza, washirika wa kibiashara na wengineo ambao hufanyakazi na Kampuni hii. Taarifa za kibinafsi ambazo hazijalindwa zinaweza kutumiwa kufanya uhalifu wa kudanganya utambulisho na kuwadhuru watu binafsi. Tumejitolea kulinda taarifa hii na ufikiaji, matumizi na ufichuzi wake ni wakati tu inapohitajika katika utenda kazi wetu.

## PATA KUFAHAMU

### TAARIFA YA KIBINAFSI INAYOTAMBULISHA

**Aina nyingi za taarifa inayotambulisha ya kibinafsi imelindwa na sheria na sera yetu, kama vile *Taarifa Inayotambulisha Kibinafsi* (PII) ambayo inauwezo wa kutumika kumtambulisha mtu fulani.**

**Mifano ya PII inajumuisha:**

- **Nambari za akaunti za benki.**
- **Tarehe za kuzaliwa.**
- **Nambari za kadi za malipo.**
- **Anwani za baruapepe.**
- **Taarifa za kibinafsi za matibabu.**
- **Nambari za simu.**
- **Anwani za makazi.**
- **Nambari za bima ya uzeeni.**

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Usiri ya California
- Sera ya Usiri wa Ndani
- Sera ya Usiri
- Sera ya Mwenendo Kazini

## Tenda Linalofaa

- **Fuata sheria na michakato yetu.** Uthibiti wa usiri wa data unahitaji makampuni kuanzisha michakato inayofaa ili kulinda PII. Kampuni yetu hudumisha michakato iliyo fanisi zaidi ili kulinda taarifa hii. Ikiwa kwa bahati mbaya utaona PII, irejeshe mara moja kwenye idara inayofaa ya Kampuni au ilete kwa msimamizi.
- **Ichukulie hiyo taarifa ya kibinafsi ya wengine kwa makini.** Ni lazima ulinde hiyo taarifa ya kibinafsi ya memba wa timu wa sasa na wa zamani, watuma maombi ya kazi, wasambazaji bidhaa, wateja, watuamiaji bidhaa na washirika wengine wa kibiashara kwa kiwango sawia cha ulinzi kama kile ungetumia kulinda yako.
- **Tumia taarifa ya kibinafsi ya memba kwa malengo yanayohusiana na kazi pekee.** Memba wa timu ni lazima apatiane ruhusa ya kutumia taarifa yake kwa malengo mengine.
- **Tumia taarifa za kibinafsi za washirika wa kibiashara na wengineo kwa makini.** Lazima itumike kwa malengo halali ya kibiashara na kamwe isishirikiwe na yeyote – ndani au nje ya Kampuni hii – pasipo idhini.
- **Ripoti haraka ufikiaji wowote usio wa kimakusudi au usiofaa, matumizi au ufichuaji.** Huenda kukawa na sheria na mipangilio ya muda inayotumika.

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Mojawapo wa wafanyikazi wenzangu alipata mwana. Wachache wetu kwenye idara wangependa kumtumia zawadi, lakini hatujui anwani ya makazi yake. Je, ninaweza kumwitisha Raslimali Watu hiyo anwani?**

**J** La. Hali kupeana zawadi kwa tukio maalum la kimaisha ni onyesho njema, hauwezi kuitisha Raslimali Watu akupe anwani ya mfanyikazi mwenza, kwa maana hili sio ombi linalohusiana na kazi. Hata hivyo, ikiwa mtu fulani ana nambari yake ya simu, unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja akupe anwani yake. Huenda ikaharibu lile shitukizi, lakini utajua moja kwa moja kutoka kwake ikiwa angependa kushiriki anwani yake.

# H KUJITOLEA KWETU KWA KUTENDEANA HAKI KWA WATEJA NA WASHIRIKA WA KIBIASHARA

**Hormel Foods haiwezi kufanya kazi na kufaulu bila ya usaidizi wa washirika wa nje. Sisi huhusika kwa haki na washirika wetu wa kibiashara na wateja, kwa sababu tunadhamini na kutambua majukumu yao muhimu katika uzalishaji na mauzo ya bidhaa zetu za ubora.**

## Kulinda Ushindani Huru na wa Haki

Tunashindana ili kushinda kwa haki, uaminifu na uadilifu. Kujitolea kwetu daima kufuata zote mbili sheria na nia yake ya sheria za kukosa imani na ushindani hutumika kila mahali ambako tunafanya biashara. Hatuchukui fursa isiyo ya haki dhidi ya mteja yeyote, mshirika wa kibiashara au mshindani kupitia kwa kutoaminika, matumizi mabaya ya taarifa, utenguzi wa ukweli au desturi zingine za kibiashara zisizo za haki.

## Tenda Linalofaa

- **Iga sheria ya kiulimwenguni.** Tendea washirika wetu wa kibiashara na wateja jinsi ungependa kutendewa. Endesha mahusiano haya kwa heshima kwa wote, uaminifu na haki, na bila ubaguzi. Tendea wateja haki unapojadiliana kuhusu uwekaji bei na mipango ya uuzaji.
- **Jifunze na ufuate sheria.** Fahamu ni nini unaweza na usichoweza kwa ushindani chini ya sera zetu na sheria. Usiwahi kukiuka sheria za kukosa kuaminika au sheria za ushindani popote ulimwenguni ambako tunafanya biashara. Epuka hata mwonekano wa kutotenda haki. Hatari kubwa ya ukiukaji wa sheria hutendeka wakati tunapotangamana na washindani.
- **Shindana kwa haki.** Epuka desturi za ufanyaji biashara usio wa haki au wa udanganyifu. Usitende lolote ambalo linaweza kuonekana kama kuzuia ushindani. Fanya tu madai ya kweli kuhusu bidhaa zetu na uwezo. Fanya vivyo hivyo kwa ofa za washindani wetu.
- **Chagua kwa hekima.** Fanya maamuzi ya ununuzi au mauzo tu kwa ubora, thamani na huduma kwa mteja. Usiwahi kufanya uamuzi wako kuonekana kuwa umeshawishiwa isivyofaa.
- **Ongea.** Wasiliana na Idara ya Kisheria au ya Uzingatiaji wa Maadili kwa maswali au mashaka kuhusu desturi za ufanyaji biashara.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera na miongozo ya Kutoaminika ya Shirika la Hormel Foods

PATA KUFAHAMU

### SHERIA ZA USHINDANI NA KUTOAMINIKA

**Sheria za ushindani ulimwenguni, zinazoitwa sheria za kukosa imani nchini Marekani, ni pana na ngumu. Sheria hizi hubadilika kulingana na hali, lakini zifuatazo ni shughuli ambazo hatufaikufanya na ni lazima turipoti haraka kwa Idara ya Ndani kwa ajili ya mwongozo:**

- **Makubaliano au ufahamu pamoja na washindani kuhusu uwekaji bei, mapunguzo au mipango ya kibiashara.**
- **Kukubaliana na washindani kugawana au kuthibiti wateja, wasambazaji bidhaa, maeneo ya kuuza, bidi au safu za bidhaa.**
- **Kukubaliana na washindani kukataa kufanya biashara na baadhi ya wasambazaji bidhaa au wateja.**
- **Kujadilia na washindani wa sasa au uwekaji bei, masharti ya mauzo, mipango ya kimkakati au gharama.**
- **Kutoa mwonekano kwamba uamuzi wa ushindani ulishawishiwa na mshindani.**

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S Jirani yangu hufanyia kazi mshindani wa Hormel Foods. Kwa kuwa sisi sote hufanya kazi katika mauzo kwenye makampuni yetu, wakati mwingine huwa tunaongea kijamii kuhusu yanayojiri kwenye sekta. Ni jana tu alipendekeza kubana orodha yetu ya bidhaa kwenye maeneo yetu yanayoambatana ili kila mmoja wetu apate nafasi kubwa zaidi kwa wauzaji wetu wakuu. Nilisema nitafikiria kuihusu, lakini ni vizuri kufanya hivyo?**

J La. Huku ni kuingilia safu za bidhaa na maeneo, ambako kutakuwa ni ukiukaji wa sheria ya kutoaminika. Ni hatari hata kujadili mpango huu, wacha hata kuutekeleza. Jirani yako anaweza kutafsiri "kufikiria kwako kuihusu" kama makubaliano yasiyo rasmi ya kuendelea. Ni bora usiwahi kujadili kazi na mshindani wako, au ikiwa ni lazima, idumisheni katika viwango vya juu zaidi na muepuke mada nyeti kama vile kubadilishana nafasi ya rafu na safu za uzalishaji bidhaa. Katika muktadha wa kikundi, fanya "kuondoka kwa makelele" ikiwa majadiliano yanageukia mada zinazohusiana na kubana ufanyaji biashara uhuru. Hii inamaanisha unapaswa kupinga kujadili mada hiyo, na ikiwa uko katika mkutano wa kawaida, uliza kwamba pingamizi lako liandikwe kwenye kumbukumbu za mkutano. Kisha ondoka mkutanoni na uwasiliane na Idara ya Kisheria kwa mwongozo haraka iwezekanavyo.

# Kushirikiana na Wahusika wa Tatu wenye Uadilifu

Washirika wetu wa kibiashara – wasambazaji bidhaa, watoa huduma, makandarasi, wauzaji wa jumla na washirika wa biashara za pamoja – hutekeleza jukumu muhimu katika mafanikio ya biashara yetu. Tunatafuta kushirikiana na wahusika wa tatu ambao hufanya kazi kwa uadilifu na kufuata viwango vya juu zaidi vya nidhamu. Wengi wa washirika wetu wa kibiashara wanaotarajiwa hupitia mchakato mahususi ili kuhakikisha kwamba uhitimu wao na uzingatiaji wa mambo ambayo Kampuni inathamini. Mahusiano haya hufuatiliwa kwa ajili ya uadilifu endelevu.

## Tenda Linalofaa

- **Chagua mshirika wa kibiashara kwa hekima.** Fanya uamuzi wako kwa kuzingatia hitimu zao tu. Lenga hitimu zao, uadilifu na utofauti katika mchakato wa kuchagua. Usishawishiwe na mahusiano yao ya kibinafsi, upendeleo wako mwenyewe au fursa za kujifaidi kama mtu binafsi.
- **Fanya mapitio rasmi.** Wasambazaji wapya wa bidhaa na washirika wengine wa kibiashara wanaotenda kwa niaba yetu mara nyingi ni lazima wapitie uchunguzi wa kina wa kabla ya kandarasi. Fuata michakato yetu ya uidhinishaji wa mshirika wa kibiashara.
- **Fuatilia mahusiano yanayoendelea.** Kuwa mwangalifu kwa ishara mbaya ambazo huenda zikajumuisha shughuli mbaya na fisadi.
- **Elimisha washirika wa kibiashara.** Wasaidie kuelewa majukumu yao, ikijumuisha wale wanaohusika na maadili yetu na viwango vya uzingatiaji na kandarasi zao.
- **Fahamu majukumu yako ikiwa unafanya kazi na idara ya serikali.** Ikiwa unafanya kazi na serikali au biashara ambayo inamilikiwa au kudhibitiwa na serikali uko na jukumu la kuelewa, kufahamu na kufuata sheria na kanuni husiani na mahusiano haya. Hii pia inatumika wakati unapofanya kazi na mamlaka za udhibiti.
- **Ongea.** Fahamisha Idara ya Sheria au Maadili na Uzingatiaji kuhusu mhusika yeyote wa tatu ambaye huenda hatimizi viwango vyetu na matakwa, au wakati unapogundua ishara mbaya.



PATA KUFAHAMU

### ISHARA MBAYA ZA MHUSIKA WA TATU

**Ni "ishara mbaya" ya ujiendeshaji mbaya ikiwa mhusika wa tatu anayefanya kazi kwa niaba ya Kampuni atafanya lolote kati ya haya:**

- **Anaomba kiasi chochote cha pesa ili apate au adumishe biashara, au asuluhishe tatizo.**
- **Anaomba ya kwamba malipo yafanywe kwa kampuni husiani.**
- **Anawasilisha ankra bila maelezo ya kutosha au ambayo hayalingani na kandarasi.**
- **Anatuma maombi yenye nyaraka hafifu au anaitisha pesa za matumizi yenye maswali.**
- **Anaomba Kampuni itayarishe aina yoyote ya nyaraka gushi (k.v., ankra).**

### SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Ninasimamia duka ndogo la usambazaji bidhaa ambalo limefanya kazi vizuri na Hormel Foods kwa miaka mingi. Lakini mwaka jana, duka hilo la kusambaza bidhaa lilinunuliwa na mambo yamebadilika. Kwa sasa ninapokea ankra nyingi zilizofikia muda wa kulipwa ambazo hazina maelezo ya bidhaa, na nyenzo za ubora wa chini na bei za juu zaidi ambazo haziambatani na kandarasi ya sasa. Je, ninapaswa kushughulikia haya vipi?**

**J** Masuala uliyotaja ni ishara mbaya ya ujiendeshaji mbaya. Kwanza, wasiliana na mwasiliani wako kule kwenye duka la usambazaji bidhaa upate maelezo na suluhu la masuala haya. Ikiwa majibu hayo hayaridhishi, wasiliana na Manunuzi ya Shirika la Hormel Foods au Idara ya Kisheria kwa hatua zitakazofuata.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Kupinga Ufisadi

# Kukusanya na Kulinda Taarifa ya Mhusika wa Tatu

Huwa tunakusanya aina nyingi za taarifa husiani na wahusika wa tatu. Kulinda mali ya kiakili na taarifa nyeti za washirika wetu wa kibiashara ni muhimu kwetu, na tunaifanya kwa uadilifu huku tukilinda taarifa zetu wenyewe. Kukusanya ujasusi wenye ushindani ni desturi halali ya kibiashara. Huwa tunapata data hii kihalali kisheria na kwa uadilifu – sio kamwe kupitia ulaghai, kugushi au kudanganya.

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S Nilihudhuria kongamano la tasnia ambako nilipata nyaraka sakafuni ambayo ilionekana kama mpango wa kimkakati wa mshindani wetu wa mwaka ujao. Nilitaka kuirudisha kwa huyo mshindani, lakini mkutano ulikuwa umeisha na hakuna yeyote kutoka kwa kampuni hiyo alikuwa angali hapo. Kwa hivyo niliibeba nyumbani, nikajiepusha kuisoma, na nikaikatakata. Je, hilo lilikuwa ndilo jambo njema kufanya?**

J Ndio, ulifanya jambo lililofaa. Ni jambo lile tungependa washindani wetu wafanye ikiwa mpango wa mkakati wetu ungefika mikononi mwao. Jambo linalofuata ni kufahamisha Idara yetu ya Kisheria kuhusu suala hili ili mshindani anaweza kufahamishwa kuhusu hali yenyewe na jinsi ulivyolishughulikia.

## Tenda Linalofaa

- **Dumisha taarifa nyeti kwa usiri.** Linda hiyo taarifa ya kisiri na haki za mali ya kiakili za washirika wetu wa kibiashara na washindani. Hii inajumuisha taarifa ya wahusika wa tatu isiyo ya umma na ujasusi wa kiushindani kama vile orodha ya bei, mikakati, makubaliano, mali ya kiakili na taarifa zingine za kisiri za kibiashara.
- **Tumia njia zingine za kimaadili pekee kukusanya ujasusi wa kiushindani.** Egemea machapisho, ripoti za uchambuzi, tovuti, mitandao ya kijamii, vyanzo vya taarifa kwenye sekta na vyanzo vingine vya umma ili kukusanya taarifa. Usiwahi kujihusisha na wizi, udukuzi au udanganyifu ili kupata ujasusi wa ushindani. Ikiwa kwa bahati mbaya utapatana na taarifa hii na haujui iwapo ilikusanywa vyema, wasiliana na Idara ya Kisheria ya Hormel Foods haraka kwa mwongozo.
- **Kuwa na tahadhari ya chanzo cha hiyo taarifa nyeti ya ujasusi.** Kuwa mwenye tahadhari unapokubali taarifa ya ushindani kutoka kwa wahusika wa tatu. Fahamu vyanzo vyake na uwe na hakika ya kwamba taarifa zenyewe hazijalindwa na makubaliano ya kutofichua au usiri, sheria za siri za ufanyaji biashara. Usiwahi kukubali taarifa nyeti ya ushindani moja kwa moja kutoka kwa mshindani.
- **Heshimu majukumu ya usiri.** Heshimu wajibu wa wengine wa kuweka kwa siri taarifa ya ushindani ambayo lazima walinde. Usiwahi kumwekea mkazo mshindani au mhusika wa tatu akiuke majukumu ya kutofichua taarifa.
- **Ongea.** Ibua mashaka yoyote kuhusu kulinda taarifa ya kisiri ya mhusika wa tatu au kusanya ujasusi wa ushindani kwa Idara ya Kisheria.

# Kutangaza Bidhaa Zetu kwa Uadilifu

Tumejitolea kwa utangazaji wa kikweli, desturi za mauzo na uuzaji ambazo ni za kuheshimu wateja wetu. Hii inajumuisha uwekaji sahihi wa lebo kwenye bidhaa, ambao unatimiza viwango vya serikali na kuashiria uadlifu wa Kampuni yetu. Ni lazima daima tuwasiliane kwa usahihi na kwa uaminifu wakati tunatangaza bidhaa zetu katika mfumo wowote, tukifanya madai yanayoweza kudhibitishwa kwa misingi ya ukweli.

## Tenda Linalofaa

- **Kuwa mkweli.** Wapatie wateja taarifa wazi kueleweka na sahihi ili kuwasaidia kufanya maamuzi ya ununuzi kwa ufahamu. Kamwe usiwasilishe vibaya bidhaa au kufanya madai ya urongo kuhusu washindani wetu.
- **Zingatia sheria zinazolinda watumiaji wa bidhaa zetu.** Memba wa timu wanaofanya kazi katika mauzo, uuzaji au kutangaza bidhaa ni lazima wahakikishe kwamba bidhaa za kutangazwa zinazingatia sheria husiani na taarifa za bidhaa, uwekaji bei na utangazaji wa kulinganisha. Lebo za bidhaa zetu lazima zizingatie matakwa yote ya serikali na viwango wa Kampuni vya usalama wa bidhaa, lishe na ubora wa juu.
- **Ongea.** Ikiwa uko na swali au unajua ukiukwaji unaowezekana wa sera yetu ya kutangaza, uuzaji, mauzo au uwekaji lebo wa bidhaa, wasiliana na nyenzo mojawapo ya Kampuni iliyopatianwa katika Kanuni hii.

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Kundi langu linatengeneza lebo ya bidhaa ya nyama ya nguruwe ambayo imebuniwa yenye chumvi kidogo zaidi. Baadhi katika kikundi wanataka kuongeza beramu pale juu ya lebo yenye "Mpya! Chumvi kidogo" lakini sina hakika kama hilo ni sawa. Je, tunaweza kuifanya?**

**J** Pengine. Kuna viwango vya serikali kuu kwa matumizi ya maneno "chumvi kidogo" kwenye lebo. Ikiwa kiwango cha chumvi kwenye hiyo bidhaa mpya kingali kiko juu na kushindwa kufikia viwango hivi, huenda unaweza kusema "chumvi kidogo" kwenye uwekaji lebo.  Chunguza kutoka kwa Idara ya Kisheria ya Hormel Foods au Mambo ya Uthibiti, Uwekaji lebo na Kubuni bidhaa ili kupata njia bora ya kuweka lebo kwenye bidhaa.

# Kuepuka Migonganoya Kimaslahi

Tumejitolea kuweka kando maslahi yetu wakati yanashindana na yale ya Kampuni hii. Hii inajumuisha kutotumia nafasi zetu kwa kujifaidi kibinafsi au kusaidia familia zetu na marafiki. Ikiwa uko katika hali ambayo huenda kuwa na uwezekano wa mgongano wa kimaslahi, ni lazima ufichue.

**INAVYOMAANISHA**

### Mgongano wa Kimaslahi

M *gongano wa Kimaslahi* hutokea wakati hali zako za kibinafsi zinahitilafiana, au kuonekana kuhitilafiana, na uwezo wako kufanya maamuzi yakini kwa ajili ya Kampuni. Hili hufanyika wakati wewe, rafiki wa karibu au memba wa familia hufaidi kibinafsi, kifedha au vinginevyo, kutokana na uamuzi wako. Kufeli kufanya maamuzi mema katika hali hii kunaweza kuharibu imani ya umma kwa Kampuni yetu, kudhuru uwezo wetu wa kuhudumia wateja wetu.

PATA KUFAHAMU

## MIFANO YA MGONGANO YA KIMASLAHI

**Hali nyingi zinaweza kusababisha mgongano wa kimaslahi. Hatuwezi kuiorodhesha yote, lakini hii hapa baadhi ya aina ya mifano ya kawaida zaidi:**

- **Mahusiano ya kibinafsi** kama vile memba wa familia, kuchumbiana au kuwa na uhusiano wa karibu na mshirika wa kibiashara, mshindani, mteja au memba wa timu ambaye huripoti kwako.
- **Kazi za nje** au mahusiano, mara nyingi zaidi na washirika wa kibiashara, washindani au wateja.
- **Uwekezaji wa Kibinafsi** ambao ni mkubwa vya kutosha kushawishi maamuzi yako ya kibiashara au huenda ikaonekana kufanya hivyo.
- **Fursa za shirika** ambazo utagundua kupitia kwa kuajiriwa kwako kwenye Kampuni na ambazo unafuatilia kwa kujifaidi kibinafsi badala ya kuweka maslahi ya Kampuni kwanza.
- **Uanachama wa Bodi** katika shirika lingine, iwe ni chombo cha kifaida au kisicho cha kifaida, wakati uhusiano huo utajenga mwonekano wa mgongano na operesheni zetu.

## WAKATI WA KUTAFAKARI MAHUSIANO YENU

**Kuna visababishi vya kawaida ambavyo husababisha memba wa timu kutathmini mahusiano yao kwa ajili ya mgongano wa maslahi. Mizozo inaweza kuibuka wakati:**

- **Wewe ni mgeni katika Kampuni hii.**
- **Una jukumu jipya ndani ya Kampuni hii.**
- **Memba wa timu ni sehemu ya mchakato wa uchaguaji wa mhusika wa tatu atoaye huduma.**
- **Rafiki yako wa karibu au memba wa familia anapata kazi na chombo ambacho hufanya biashara na Kampuni.**
- **Kuna biashara ya kufanya pamoja, kuungana kwa makampuni au utwaaji wa kampuni.**
- **Mabadiliko ya kimkakati hutokea ndani ya shirika hili.**



## Tenda Linalofaa

- **Kuwa mwenye kujituma.** Kuwa mwenye kufahamu hali ambazo huenda zikajenga mgongano wa maslahi na uziepuke, ikiwezekana. Ikiwa hauwezi kuondokea mgongano wa maslahi, uzungumzie na msimamizi wako au Idara ya Kisheria.
- **Kuwa Mhalisia.** Tumia uamuzi mwema na usiruhusu chochote kihitilafiane na uwezo wako wa kufanya maamuzi ya maslahi bora ya Kampuni. Usipatiane biashara kwa mtu wa karibu nawe au kwa kampuni inayomilikiwa na mtu ambaye uko na uhusiano wa kibinafsi naye. Jiondoe kutoka kwa mapitio yoyote ya ofa kama hizo.
- **Ongea.** Zungumza na msimamizi wako au chanzo kingine kilichopeanwa katika Kanuni hii kuhusu hali yoyote ambayo huenda ikwa mgongano wa kimaslahi kwako au mfanykazi mwenza, ikijumuisha hali ambazo huleta mwonekano wa mgongano wa kimaslahi. Ufichuaji haimaanishi itapigwa marufuku. Mara nyingi mgongano wa kimaslahi unaweza kushughulikiwa na kusuluhishwa.

### SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Dada yangu anamiliki shamba ndogo ambako hulea na kuuza nguruwe wa ubora wa juu kwa bei za wastani. Je, ninaweza kupeana jina langu kwa wenzangu ambao huchagua wanaouzia Hormel Foods?**

**J** Kampuni daima inatafuta washirika bora zaidi wa kibiashara, na dada yako huenda anafaa vigezo vile. Ni sawa kupeana jina lake pamoja, lakini hauwezi kuwa sehemu ya ule mchakato wa uchaguaji. Pia, ikiwa wewe ni kiongozi wa Kampuni hii, tambua kwamba pendekezo kutoka kwako yaweza kuonekana kama amri kwake kupewa kandarasi. Kuwa mwangalifu usije ukatuma ujumbe huu. Kwa kuongezea, iweke wazi kwamba ni lazima yeye ashindanie kupata ile fursa ya kibiashara.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Mgongano wa Kimaslahi na Fomu ya Ufichuaji

# Kupeana na Kupokea Zawadi na Hisani

Zawadi kiasi na zisizo za mara kwa mara na hisani za kibiashara zinaweza kuwa ishara zinazofaa za nia njema na husaidia kujenga mahusiano. Hata hivyo, wakati mwingine hisani kama hizo zinaweza kufumba maamuzi yanayofaa ya kibiashara. Hazifai kamwe kupeanwa au kupokelewa ili kushawishi fursa ya biashara au maamuzi ya kiuthibiti na kamwe hazifai kuwa za kuzidi mno au za mara nyingi. Zawadi au hisani inaweza kuonekana kama mgongano wa maslahi au hata hongo haramu katika hali zingine. Tunajisatiti kuzingatia maadili ya biashara yoyote hisani ya kudumisha sifa njema ya Kampuni na kuwatumikia vyema wateja wetu.

**INAVYOMAANISHA**

## Hisani za Kibiashara

*Hisani za kibiashara* ni vitu vinavyohusiana na biashara au huduma za thamani zinazopatianwa au kupokelewa kutoka kwa mtu fulani ambaye hufanya kazi na Kampuni au yule anayekusudia kufanya hivyo hapo baadaye. Hisani hizi hujumuisha zawadi, fadhila, usafiri na wakati mwingine hata shughuli ya kijamii au ishara ya upole. Mifano inajumuisha milo, hafla za michezo, hafla za sarakasi, mapokezi na hafla za kijamii zilizodhaminiwa au kuandaliwa na mpeanaji. Hata mlo mdogo au kinywaji kinaweza kuchukuliwa kuwa ni hisani.

PATA KUFAHAMU

## KITU KINACHOWEZA KUKUBALIWA

**Zawadi na hisani zinazokubalika lazima ziwe:**

- **Ndogo kwa thamani, sio zaidi ya USD $100 kwa kila zawadi.**
- **Chini ya USD $250 kwa jumla kutoka kwa chanzo kimoja katika mwaka mmoja.**
- **Inayofaa, sio haramu kisheria au ya kuudhi.**
- **Inayoambatana na sera za Kampuni na desturi za kawaida.**
- **Huru kutokana na tarajio la kupata kitu fulani baadaye.**

## Tenda Linalofaa

- **Zingatia sera zile.** Zingatia sera zetu na zile za shirika la mpokeaji wakati wa kupeana au kupokea zawadi yoyote ya kibiashara au hisani. Kujitumbuiza kibiashara au kwa kawaida kumeruhusiwa na wawekezaji wengi, wateja na wengine ambao hufanya kazi na Hormel Foods ikiwa inaambatana na sera za Kampuni na desturi za kawaida.
- **Kataa hisani zinazokusudiwa kushawishi.** Hakuna zawadi au hisani inayohusu mtu anayefanya kazi na Kapuni inaweza kupeanwa au kukubaliwa iwapo inashawishi au imekusudiwa kuathiri maamuzi ya kibiashara. Epuka hata mwonekano wa ushawishi. Kwa mfano, usiwahi kubadilishana hisani zozote wakati wa mchakato wa ufanyaji mnada.
- **Usiwahi kupeana au kupokea pesa taslimu au kibadala kinachotoshana na pesa.** Hii inajumuisha kadi za zawadi, haijalishi thamani yake. Hizi zinachukuliwa kuwa vibadala vinavyotoshana na pesa.
- **Kataa kabisa hisani zisizofaa.** Hili huenda likawa la usumbufu kwako au la kuudhi kwa mpeanaji, lakini wakati zawadi au hisani haifai (kwa mfano, chakula cha usiku katika eneo la watu wazima kujitumbuiza), nia lazima ukatae kwa upole.
- **Kuwa na tahadhari kwa maafisa wa serikali.** Wakati unafanya kazi na afisa wa serikali, ni lazima ufuate kanuni zote za serikali ndogo na serikali kuu kuhusiana na hisani za kibiashara, pamoja na sera ya Hormel Foods. Ni muhimu kushauria na Idara ya Kisheria au Idara ya Maadili na Uzingatiaji kabla ya kupeana zawadi au kumtumbuiza afisa wa serikali.
- **Ongea.** Uliza kuongozwa wakati hauna hakika kuhusu la kufanya. Pata ushauri wa msimamizi wako au Idara ya Maadili na Uzingatiaji ikiwa uko na swali au mashaka kuhusu hali fulani inayohusu zawadi au hisani.

## Maswali na Hisani

| Je, Ninaweza kubali Hisani Hii? | Jibu ni... |
|---|---|
| Makaribisho kwa hafla ya michezo ya kataalamu kama mgeni wa msambazaji wa bidhaa ambaye anahudhuria hafla ile. | **Ndio.** Huku ni kujitumbuiza kwa kibiashara au kwa kikawaida na kunaambatana na desturi za kawaida za Kampuni. Hata hivyo, ikiwa kuna thamani ya USD $100 au zaidi na yule msambazaji wa bidhaa hahudhurii, itachukuliwa kuwa zawadi isiyokubalika. |
| Kadi ya zawadi au zawadi ya kushindwa katika uchoraji wa bila mpangilio katika kongamano la kisekta. | **Ndio.** Zawadi au kadi ya zawadi ya kushindwa katika uchoraji wa mpangilio haichukuliwi kuwa zawadi ambayo inaweza kukushawishi na inaweza kukubaliwa. |
| Zawadi kadhaa za thamani ndogo kutoka kwa mwanakandarasi mmoja ya jumla ya zaidi ya $250 kwa mwaka mmoja. | **La.** Hili linachukuliwa kuwa utoaji zawadi usiofaa. Mshirika yeyote binafsi anaweza tu kupeana vitu vya zawadi ambazo zinafikia hadi jumla ya USD $250 kwa thamani kwa mwaka. |
| Tiketi kwa hafla ya kujitumbuiaza inayogharimu hadi jumla ya USD $80 kwa thamani kutoka kwa mteja ambaye hahudhurii. | **Ndio.** Zawadi ya chini ya $100 ni ndogo kwa thamani na inaweza kukubalika. Mteja huyo sio lazima ahudhurie. |
| Usafiri na malazi yaliyolipiwa na msabazaji bidhaa anayetarajiwa ya kutalii kituo chake na maeneo ya uzalishaji. | **La.** Ikiwa imeidhinishwa awali na Hormel Foods, Kampuni italipia gharama za safari hiyo. |
| Tunda kubwa la likizo, jibini na vitafunio kutoka kwa msambazaji bidhaa ambayo inaonekana kuwa ya ziadi ya USD $100 kwa thamani. | **Ndio.** Zawadi zinazoharibika haraka ambazo haziwezi kurejeshwa zinaweza kupokelewa ikiwa zitashirikiwa na wengineo kwenye idara yako. Hata hivyo, ikiwa hii ni sehemu ya msururu wa zawadi unaofikia zaidi ya jumla ya USD $250 kutoka kwa mtoa huduma mmoja, inafaa kukataliwa. |



NYENZO

### Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Kupambana na Ufisadi
- Sera ya Kusafiri Kibiashara
- Sera za Usafiri za Kampuni na Michakato
- Sera ya Ripoti ya Gharama
- Sera ya zawadi, Zawadi za Kujishindia na Tuzo

# KUJITOLEA KWETU KULINDA KAMPUNI YETU

**Afya ya Kampuni yetu imejengwa juu ya sifa imara za uadilifu. Kila maamuzi ya kibiashara yanayofanywa na kila memba wa timu lazima yaunge mkono malengo haya, na memba wote wa timu ni lazima waweke kando kujifaidi kwa kibinafsi kwa ajili ya fanaka ya Kampuni.**

## Kudumisha Uadilifu Wetu wa Kifedha

Kila mmoja wetu anacheza katika kutekelezesha afya ya kifedha ya Kampuni hii. Kama kampuni ya hisa kwa umma, tuna matakwa, sheria na kanuni za uthibiti ambazo zimesimamiwa na Tume ya Hisa na Ubadilishanaji (Securities and Exchange Commission, SEC) ya Marekani na Soko la Hisa la New York. Tunategemea sera zetu za uhasibu, michakato ya vidhibiti vya ndani na ufichuaji ili kuhakikisha usahihi wa nyaraka zetu za kifedha. Ni muhimu kwamba uwekaji faili kwa umma na ufichuaji wa wawekezaji ni sahihi, kamili na unaoeleweka. Tunadumisha uadilifu wetu wa kifedha kupitia ufanyaji maamuzi mema na hatua za kiuadilifu.

PATA KUFAHAMU

### URIPOTI WA SERIKALI

**Serikali na mawakala wa kuorodhesha hisa, ndani na nje ya Marekani, wana matakwa mahususi kwa ajili ya ripoti na uwekaji faili zinazowasilishwa na makampuni. SEC na Huduma ya Ndani ya Mapato ya Marekani ni mifano ya mawakala hawa.**

**Wakurugenzi na memba wengine wa timu ambao huandaa, kusimamia, kupitia au kuthibitisha ripoti hizi na uwekaji faili ni lazima wahakikishe kwamba mawasilisho yao ni sahihi, kamili na ya kuaminika. Ni lazima pia watimize matakwa yote ya serikali ya sera za kuripoti na kufichua taarifa kuhusiana na Kampuni yetu. Dosari yoyote yaweza kuwa na matokeo mabaya sana. Yeyote atakayekuwa na ufahamu wa taarifa ambayo inaweza kuathiri usahihi wa uwekaji faili kwa umma wa Kampuni au ufichuaji anapaswa Kuongea haraka na Afisa Mkuu wa Uzingatiaji wa Hormel Foods.**

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Uanishaji wa Karatasi ya Mizania

## Tenda Linalofaa

- **Elewa jukumu lako kuelekea uadilifu wa kifedha.** Ikiwa wewe unasimamia mali isiyohamishika ya kampuni, gharama, bajeti, kauli za kifedha, uwekaji faili au ripoti za serikali, hakikisha unazishughulikia kwa makini, kwa usahihi na uaminifu.
- **Fuata matakwa yote ya kisheria na vidhibiti vyetu vya kifedha.** Peana taarifa ambayo ni kamili, sahihi, kwa wakati unaofaa na kwa njia wazi. Zingatia vidhibiti vyetu na michakato na sera za ndani ya kifedha, uhasibu na ukaguzi.
- **Hakikisha kwamba miamala na mauzo yamerekodiwa vyema.** Uwekaji mwema wa nyaraka lazima uunge mkono miamala yote ya kifedha. Ni lazima ziwekewe nyaraka katika kipindi kinachofaa cha uhasibu na katika akaunti inayofaa. Usijaribu kujazilia bajeti kwa kuzirekodi mapema au baadaye.
- **Heshimu mchakato wa ukaguzi.** Shirikiana na wakaguzi, wa ndani na wa nje.
- **Ripoti dosari au mashaka haraka.** Ongea haraka iwezekanavyo kuhusu makosa yoyote au dosari kwenye rekodi zetu za kifedha, uhasibu au ukaguzi.

### SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Msimamizi wangu aliniomba kurekodi ingizo ambalo linaonekana kuingiza kiasi kasoro ya thamani ya mali isiyohamishika katika vitabu vyetu. Je, nifanye vile msimamizi wangu anasema?**

**J** La. Kwa kuweka kiasi kasoro cha thamani ya mali isiyohamishika ukijua ni wazi kwamba ni urongo na kunaweza kuwa ulaghai. Kwanza, zungumza na msimamizi wako kuhusu mashaka hayo. Anaweza kuwa alikuwa amefanya kwa makosa. Ikiwa hili ni la usumbufu zaidi, au ikiwa msimamizi wako anajaribu kutetea ombi hilo, pandisha mashaka yako hadi kwa mojawapo ya nyenzo za Kampuni zilizoorodheshwa katika Kanuni hii. Dosari katika rekodi zetu za kifedha lazima ziepukwe au kusahihishwa.

# Kusimamia Vitabu na Rekodi Zetu

Rekodi za Kampuni na nyaraka hujenga historia inayoendelea ya shughuli za biashara zetu. Wawekezaji, wateja, washirika wa kibiashara, maafisa wa serikali na wafanyakazi wenza hutegemea usahihi wa vitabu na rekodi zetu. Rekodi za uendeshaji, za fedha na za kibiashara ni lazima ziwe za kuaminika ili zionyeshe picha yenye kuaminika ya mambo yetu ya biashara.

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S Mmoja wa wafanyakazi wenzangu mara kwa mara huwasilisha ripoti zake za gharama baada ya tarehe ya kukamilisha kazi, na nimemwona akitengeneza nyaraka ili kuhalalisha baadhi ya gharama zake. Je, msimamizi wetu ana jukumu la kugundua mambo haya?**

J Ndio na la. Msimamizi wenu anawajibika kwa kupitia ripoti za gharama za memba wa timu, lakini iwapo unafahamu mawasilisho yaliyochelewa au yasiyo kamili, uwekaji duni wa rekodi au risiti za urongo, inaweza kuwa dalili ya ulaghai. Ripoti dosari hizi zote kwa msimamizi wako.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Kupambana na Ufisadi
- Video ya Kugushi Nyaraka
- Sera ya Rekodi na Udhibiti wa Taarifa (Records and Information Management, RIM)
- Ratiba ya Ushikiliaji wa Rekodi



## Tenda Linalofaa

- **Dumisha vitabu na rekodi zinazotegemeka.** Rekodi mali zote, madeni, mapato na gharama vizuri kwa kutumia taratibu za Kampuni. Rekodi zote za Kampuni ni lazima zieleze kwa kweli miamala au shughuli zinazorekodiwa, iwe ziko katika karatasi au fomu ya kielektroniki.
- **Fuata sera zetu za usimamizi wa nyaraka na uhifadhi.** Ni lazima uhifadhi aina fulani za rekodi, kwa muda fulani bayana kwa kawaida. Sera zetu na taratibu zinadokeza ni nyaraka zipi lazima zihifadhiwe, kwa urefu wa muda gani, wakati zinaweza kuharibiwa na jinsi ya kuzitupa.
- **Zingatia ushikiliaji halali wa rekodi kisheria.** Rekodi zinazohusiana na mashtaka, ukaguzi au uchunguzi huenda zikahitaji kuhifadhiwa kwa muda zaidi kuliko kipindi cha muda kilichotajwa katika sera yetu. Wakati hilo linapotendeka, Idara ya Kisheria itatoa maagizo yakieleza kwa kina taarifa itakayowekwa na kuwepo hadi ule ushikiliaji utaondolewa. Usiwairekebishe, kubadilisha au kuharibu nyaraka zozote ambazo ziko chini ya ushikiliaji halali wa rekodi kisheria.
- **Ongea.** Uliza swali au eleza mashaka iwapo unafikiri rekodi ya biashara sio sahihi, yenye kuaminika au kudumishwa inavyofaa.

INAVYOMAANISHA

## Rekodi za Biashara

*Rekodi za Kibiashara* zinajumuisha nyaraka anuwai, kama vile ripoti za gharama, taarifa za kifedha, mipango ya uuzaji, malipo ya ankara, uwekaji wa rekodi za serikali, rekodi za uzalishaji, wahakiki wa ubora, ripoti za ukaguzi na mengi zaidi.

# Kudumisha Mali ya Kampuni Isiyohamishika

Tumejitolea kutumia mali isiyohamishika ya Hormel Foods kwa busara na kwa kusudi ambazo hufaidi Kampuni. Kila mmoja wetu ana jukumu la kibinafsi la kutumia mali isiyohamishika ya Kampuni kama ilivyokusudiwa na kuikinga kutokana na hasara, wizi, uharibifu, kutotumika vizuri na kutumia visivyofaa.

## KINGA MIFUMO YETU YA TAARIFA

- **Punguza matumizi ya kibinafsi ya simu na kompyuta za Kampuni. Shughuli kama ununuzi, mambo ya kibenki na kupitia mitandao ya kijamii zinakubalika mara kwa mara, ili mradi zisisababishe hatari za usalama au kuhitilafiana na majukumu yako ya kazi au uzalishaji.**
- **Usitumie mifumo ya teknolojia ya Kampuni kwa ajili ya michezo, kutuma barua nyingi au utani, au kwa kusudi la kuudhi au kukiuka sheria.**
- **Weka jina la mtumiaji na nenosiri binafsi.**
- **Usiruhusu wengine, ikijumuisha marafiki na familia, kutumia rasilimali zetu za teknolojia.**
- **Usitoe, kuhifadhi au kutuma maandishi yenye kuudhi.**
- **Usifungue viunganishi vya barua pepe au barua pepe ambazo zina mashaka, hata kama unajua aliyetuma.**
- **Tumia tu programu ambayo imepewa leseni sahihi.**
- **Usiwahi ongeza programu yako ya kibinafsi kwa kompyuta za Kampuni, simu au vifaa vingine bila kibali.**
- **Usitarajie faragha wakati unapotumia barua pepe, intaneti au teknolojia nyingine ya Kampuni. Kampuni ina haki ya kufuatilia utumiaji wa vifaa vyake vya kiufundi, mtandao au mifumo.**

## Tenda Linalofaa

- **Linda mali ya Kampuni kana kwamba ilikuwa yako.** Unawajibika kwa matumizi mema ya kulinda mali isiyohamishika ya Kampuni ambayo imedhaminiwa kwako.
- **Weka usalama wa kuonekana katika eneo lako la kazi.** Linda ofisi yako, kituo cha kazi na vifaa kwa kufungia vitu au kuzima mashine kabisa wakati hazitumiki. Fuata sera ya kuondoa vitu mezani – safisha meza yako kwa kuondoa nyaraka kila siku kabla ya kuondoka kwenye kituo cha kazi.
- **Omba ruhusa.** Pata idhini iliyoandikwa kabla ya kukopesha, kuuza au kutoa mchango wa mali isiyohamishika ya kampuni.
- **Ongea.** Ripoti matukio ya kukisia wizi au matumizi mabaya ya mali yetu isiyohamishika. Pia ripoti kifaa chochote ambacho kimeharibika, kisicho salama au kinachohitaji ukarabati.

PATA KUFAHAMU

## MIFANO YA MALI ISIYOHAMISHIKA YA KAMPUNI

**Kuna aina nne ya mali isiyohamishika ya kampuni. Mifano kadhaa ya kila aina inajumuisha:**

- **Ya kielektroniki – kompyuta, vifaa vya uhifadhi vya kielektroniki, mifumo ya taarifa.**
- **Ya kifedha – kadi za mkopo za kampuni, ankara, akaunti za benki, rekodi za kifedha.**
- **Taarifa – hifadhidata, faili, mali ya kiakili, fomula za bidhaa.**
- **Ya Kuonekana – viwanda, vifaa, malighafi, zana.**

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Nilimsikia meneja kwa mbali akisema kwamba alichukua zana kadhaa kutoka kwa idara yetu ya matengenezo ya kiwanda ili kutumia nyumbani mwishoni mwa juma. Alisema kwamba alirudisha zana hizi siku ya Jumatatu. Je, ninapaswa kumwambia mtu yeyote kuhusu hili?**

**J** Ndio, unapaswa Kuongea. Nyenzo za Kampuni, kama vile zana na vifaa, zinatumika tu pekee kuleta mazingira ya kazi yaliyodhibitiwa na salama kwa ajili ya memba wetu wa timu. Unapaswa kuzungumza na msimamizi wako mara moja kuhusu ulichosikia.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Miongozo ya Uhifadhi wa Data
- Sera ya Usalama wa Sekta
- Mwongozo wa Usalama wa Kipakatalishi
- Sera ya Kifaa Tamba

# Kulinda Taarifa ya Siri ya Kampuni

Mojawapo ya mali isiyohamishika yenye thamani kubwa zaidi ya Hormel Foods ni taarifa yetu ya siri ya kampuni, ikijumuisha mali ya kiakili. Tuna wajibu wa kuiweka salama na kuikinga kutokana na hasara, matumizi mabaya na ufikiaji na kufichuliwa kusikofaa.

**INAVYOMAANISHA**

## Taarifa Nyeti ya Kampuni

*Taarifa ya Usiri ya Kampuni* ni taarifa yoyote inayohusu biashara ya Hormel Foods ambayo haijawasilishwa hadharani, bila kujali makataa ya ufikiaji, utumiaji au kufichua.

*Mali ya kiakili* ni aina moja ya taarifa za kisiri. Inaweza kuwa wazo, ubunifu, uvumbuzi, uboreshaji au dhana nyingine inayomilikiwa na Kampuni.

PATA KUFAHAMU

## MIFANO YA TAARIFA YA SIRI YA KAMPUNI

**Taarifa zetu zote za siri haziwezi kuorodheshwa hapa, lakini baadhi ya mifano ni:**

- **Michakato ya Utengenezaji Bidhaa.**
- **Majadiliano ya Kuunganisha na Kutwaa makampuni.**
- **Data ya wafanyakazi.**
- **Fomula za bidhaa.**
- **Taarifa za mauzo.**
- **Siri za kibiashara.**
- **Taarifa za kifedha zisizofichuliwa.**

## Tenda Linalofaa

- **Fahamu yaliyo ya kisiri.** Data nyeti ambayo ni ya Kampuni mara nyingine huwekwa alama ya siri lakini sio kila wakati. Ni lazima uweze kutambua mambo ya usiri kwa hali yake.
- **Zingatia sera zetu.** Fikia na utumie habari za siri kwa madhumuni halali ya biashara pekee, na uilinde wakati haitumiki. Shiriki tu na wahusika walioidhinishwa kwa sababu zinazohusiana na kazi au ikiwa inahitajika kisheria. Kuwa mwangalifu kuepuka kuijadili mahali ambapo unaweza kusikilizwa. Ikiwa unamiliki habari hii, lazima uirejeshe kwa Kampuni unapoombwa au wakati ajira yako imekoma.
- **Fichua ubunifu wako.** Uvumbuzi wowote, maendeleo, ubuni, au uboreshaji unayounda ambao unahusiana na biashara ya Kampuni lazima yafunuliwe kwa Kampuni kwa maandishi. Katika hali nyingi, itakuwa mali ya kipekee ya Kampuni. Ikiwa imeundwa kwa wakati wako mwenyewe, bila raslimali za Kampuni na haihusiani na biashara au utafiti wa Hormel Foods, haitakuwa ya Kampuni.
- **Tumia vifaa vilivyoidhinishwa.** Kompyuta zote na vifaa vingine, pamoja na media ya kuhifadhi (k.v., vifaa vya USB) zinazotumiwa kuihifadhi au kupata habari za siri zinapaswa kutoka kwa Idara ya Teknolojia ya Kampuni au ziidhinishwe kutumika.
- **Kulinda habari za watu wengine.** Bei ya washirika wa biashara, makubaliano na data zingine nyeti lazima zishughulikiwe kwa kulindwa kama zetu. Pia, usitumie vibaya mali ya wengine, kama vile programu.
- **Ripoti utumizi mbaya, kupoteza na kutoa taarifa.** Ongea haraka na msimamizi wako au raslimali nyingine ya Kampuni ikiwa unaamini kuwa habari za siri zimeshughulikiwa vibaya, zimeibiwa au zimepotea.



## SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Mara nyingi nafanya kazi na habari za usiri za Kampuni. Naweza kushirikiana na mmoja ambaye hufanya katika Hormel Foods?**

**J** La. Unaweza kushiriki habari hii na memba wengine wa timu ambao wanahitaji kuipata ili kufanya kazi zao. Mahitaji haya ni muhimu sana kukumbuka wakati wa kufanya kazi na aina zetu nyeti za habari za siri.

NYENZO

### Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera za Uainishaji wa Data
- Sera ya Usiri wa Ndani
- Sera za Mitandao ya Kijamii kwa Matumizi ya Kibiashara

# Kuuza Hisa na Dhamana Zingine Kisheria

Wakati wa kazi yako, unaweza kuja kupata habari juu ya Kampuni yetu au kampuni nyingine ya umma ambayo haipatikani kwa umma kwa wawekezaji wote. Habari hii inaweza kuwa ya thamani kwa wamiliki wa hisa, kwa sababu inaweza kuathiri uamuzi wao wa kununua au kuuza hisa za kampuni au dhamana. Kuuza hisa au dhamana zingine kulingana na habari hii inaitwa biashara ya ndani, na ni kinyume cha sheria.

## INAVYOMAANISHA

### Habari za ndani au za mtu wa ndani

ni habari, habari isiyo ya umma kuhusu kampuni inayouzwa hadharani inayoweza kumpa mwekezaji faida ya kifedha wakati wa kununua, kuuza, au kushikilia hisa au dhamana zingine.

### Habari ya nyenzo

ni maarifa ambayo yatakuwa muhimu kwa mwekezaji ambaye anafanya uamuzi juu ya kununua, kuuza au kushikilia hisa za kampuni. Kwa ujumla, habari hii inapotolewa hadharani, ingekuwa na athari kwa bei ya hisa za kampuni. Mifano ni pamoja na ujuzi wa kuungana au upataji, kurejeshwa kwa bidhaa, mabadiliko katika usimamizi wa watendaji, matokeo ya mapato na maswali ya serikali.

### Habari isiyo ya umma

inakuwa ya umma mara tu imesambazwa sana nje ya Kampuni kupitia machapisho au ripoti kwa SEC.


## Tenda Linalofaa

- **Elewa na ufuate sheria na sera zetu.** Usinunue au kuuza hisa, dhamana, chaguzi au dhamana ya Hormel Foods au kampuni yoyote ya umma kulingana na habari ya ndani kuhusu kampuni hiyo. Hii ni kinyume cha sheria.
- **Usiwape wengine vidokezo.** Usishiriki habari za ndani na marafiki au familia ili waweze kufanya biashara ya dhamana kulingana na dokezo. Hii ni kinyume cha sheria pia.
- **Ongea.** Ikiwa huna hakika kama kitu fulani ni habari isiyo ya umma, usishiriki na wengine au kufanya biashara ya hisa kulingana nayo. Tafuta mwongozo kutoka kwa msimamizi wako au Idara ya Sheria kabla ya kuchukua hatua yoyote.

NYENZO

### Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Biashara ya Ndani ya Shirika la Hormel Foods



# Kuwasiliana kwa Uangalifu

Wakati wowote tunapowasiliana na wengine nje ya Kampuni yetu, inatupa nafasi ya kuimarisha sifa yetu ya chapa. Hiyo ni moja ya sababu tunahakikisha mawasiliano yetu ya maneno na maandishi na wateja, washirika wa biashara na wanajamii ni weledi, sahihi na mkweli. Kila mara tumia uangalifu maalum unapoandika chochote kitakachoonekana kwa media ya kielektroniki au kutumwa kupitia barua pepe. Usiwahi kuongea kwa niaba ya Kampuni isipokuwa kama umeidhinishwa kufanya hivyo.

PATA KUFAHAMU

## KUTUMIA MITANDAO YA KIJAMII

- **Andika katika usemi wa mtu wa kwanza na utumie anwani ya barua pepe yako binafsi wakati unatuma katika mitandao ya kijamii.**
- **Iwapo utataja Hormel Foods katika mitandao ya kijamii, jitambulishe kama mfanyakazi wa Kampuni.**
- **Unawajibika kisheria kwa chochote unachoandika au kuchapisha mtandaoni.**
- **Kupeana taarifa nyeti za biashara inaweza kukuingiza wewe na Kampuni katika shinda za kisheria.**
- **Kanuni Zetu na Sera za Kampuni hutumika katika mitandao ya kijamii na nafasi za mitandao.**
- **Unaweza kuadhibiwa kwa chapisho mtandaoni ambalo ni la kukashifu, la wamiliki, la kunyanyasa au la haramu, na pia mwenendo wowote usiofaa wa mtandaoni ambao unaleta athari mbaya kwa Kampuni.**

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Mitandao ya Kijamii
- Sera ya Mitandao ya Kijamii kwa Matumizi ya Kibiashara



# Tenda Linalofaa

- **Wasiliana kwa heshima na uadilifu.** Fikiria kabla ya kuongea au kuandika, na kila wakati tumia busara. Usijiunge na shughuli za mtandaoni au barua pepe ambazo hazitakubalika kibinafsi. Machapisho yaweza kusomwa sana na washindani, wanaotafuta kazi, wasimamizi na wengine ambao wanaweza kupinga masilahi yetu. Machapisho ya Mtandaoni na barua pepe yanapaswa kuandikwa kwa weledi na wazi ili kuelezea nia yako. Tumia maneno ambayo haiwezi kutoeleweka. Kutokuwa mwangalifu jinsi unavyowasiliana inaweza kusababisha madhara kwa Kampuni.
- **Linda habari za Kampuni.** Usiwahi chapisha habari za siri za Kampuni katika mitandao ya kijamii au wakati unajibu kwa chapisho zinazohusiana na chapa ikiwa habari haijatolewa. Usitume habari iliyokatazwa, kama ilivyoainishwa kwa sera ya uainishaji wa data, kwa barua pepe bila idhini na usimbuaji sahihi.
- **Kuwa mwangalifu jinsi unavyojiendesha.** Ijapokuwa umeruhusiwa kufanya hivyo, usijiwasilishe kana kwamba unaongea kwa niamba ya Kampuni.
- **Patiana maombi ya taarifa kwa wanaofaa.** Ni muhimu kwetu sisi kutumia sauti halisi wakati tunapoongea kwa niamba ya Kampuni. Ndio sababu lazima upeleke maombi yote ya habari kwa Mawasiliano ya Kampuni au Mahusiano ya Wawekezaji ili wale ambao wameidhinishwa kusema hadharani kwa niaba ya Kampuni waweze kushughulikia uchunguzi.
- **Ongea.** Ikiwa hauna uhakika juu ya nini cha kuwasiliana na jinsi ya kufanya hivyo, wasiliana na Timu ya Mawasiliano ya Kampuni ili ujifunze kile unaweza na usichoweza kusema, na jinsi ya kuhakikisha unafanya kwa weledi.

## SWALI LA MAISHA HALISI

S **Niliona chapisho linalohusu Vyakula vya Hormel kwenye wavuti ya blogi ya tasnia ambayo najua sio kweli. Nataka kutuma sahihisho ili kuweka rekodi sawasawa. Je, hili ni vyema kwangu mie kulifanya?**

J La. Umesema kweli kwamba habari hii potofu inahitaji kurekebishwa, lakini badala ya kutuma jibu mwenyewe, peleka jambo hilo kwa timu ya Mawasiliano ya Kampuni. Memba wa timu walioruhusiwa kuongea kwa niamba ya Kampuni watafuatilia kuweka sahihisho katika blogi.

U

# KUJITOLEA KWETU KWA SHIRIKA RAIA LENYE UWAJIBIKAJI

**Kuishi kulingana na majukumu yetu kama raia wa ushirika wa ulimwengu kuna athari halisi na nzuri kwa mazingira ya asili, kwa jamii zetu na jinsi tunavyofanya biashara ulimwenguni. Tumejitolea kucheza sehemu yetu ili kufanya ulimwengu mahali pazuri.**

## Kushiriki Biashara za Kiulimwengu

Sheria za biashara za kimataifa zinaamuru wapi, jinsi na ni nani tunaweza kufanya biashara kote ulimwenguni. Sheria hizi ni pamoja na udhibiti wa forodha na uagizaji, udhibiti wa usafirishaji nje, sheria za kupinga kususia, vikwazo na vikwazo vya biashara. Ukiukaji wa sheria unaweza kubeba adhabu kubwa za kiuhalifu na jinai. Kufuata sheria hizi kunaturuhusu kufuata sheria na kuhakikisha Kampuni yetu haipati adhabu au vikwazo. Kwa njia rahisi, ni jambo linalofaa kufanya.

### INAVYOMAANISHA

#### Forodha na udhibiti wa kuagiza

tawala uingizaji wa bidhaa ndani ya nchi, pamoja na uainishaji wa bidhaa, utambulisho sahihi wa nchi asili, uwasilishaji kwa wakati na uhifadhi wa nyaraka zinazohitajika, kwa ulipaji wa ushuru na ada.

#### Udhibiti wa kuuza nje ya nchi

ni kanuni ambazo zinakataza usafirishaji wa bidhaa au habari bila leseni kwa sababu za usalama wa kitaifa au ulinzi wa biashara.

#### Sheria za kupinga ususiaji

ni sheria za Marekani zinazokataza au kuadhibu mwenendo unaounga mkono kususiwa kwa uchumi wa kimataifa. Sheria hizo zinazuia kampuni za Marekani kutumiwa kutekeleza sera za kigeni za mataifa mengine ambayo yanapingana na sera za Marekani.

#### Vikwazo vya Kibiashara

ni adhabu kibiashara na kifedha au marufuku kwa biashara iliyowekwa na serikali dhidi ya nchi zingine, watu na mashirika, kwa kuzingatia sera za kigeni na wasiwasi wa usalama wa kitaifa. Vikwazo vya kiuchumi vinakataza shughuli mbali mbali za kibiashara na taasisi zinazolengwa. Adhabu hizi sio lazima ziwekwe kwa sababu ya hali ya kiuchumi. Zaweza kutungwa kwa sababu anuwai za kisiasa, kijeshi na kijamii.

## Tenda Linalofaa

- **Zingatia sheria zote za biashara ambazo zinatumika kwa biashara yetu.** Ikiwa unafanya kazi na operesheni za kimataifa, au kwa ununuzi au uuzaji nje ya Marekani, lazima ujue na uzingatie sheria zinazotumika kwa kazi yako na usafirishaji wa bidhaa kuvuka mipaka.
- **Heshimu sheria za kibiashara za kimataifa.** Wakati mwingine inaweza kuwa haijulikani ni sheria na mazoea gani yanayotumika kwa miamala maalum ya biashara ya kimataifa. Ikiwa una maswali, haujui jinsi ya kuendelea, au unaamini mshirika wa ugavi au mshirika wa biashara anayesambaza anakiuka sheria ya biashara, wasiliana na Idara ya Maadili na Utekelezaji au Idara ya Sheria mara moja.
- **Zingatia vikwazo vya serikali.** Usifanye biashara na nchi, watu au taasisi ambazo zipo chini ya vikwazo vya kibiashara au vikwazo vya kiuchumi. Usiwahi jishughulisha na au kukuza ususiaji ambao serikali ya Marekani haiungi mkono.
- **Fuatilia wahusika wetu wa tatu.** Ugavi wa ndani na wa nje na wahusika wengine wa tatu lazima pia watii sheria. Iwapo watakiuka sheria za kibiashara, Kampuni yetu yaweza kiwajibishwa. Mara tu unaposhirikisha mhusika wa tatu, fuatilia kwa makini na kila wakati angalia chochote ambacho kinaweza kuonyesha mwenendo usiyo wa kisheria au uadilifu.
- **Ongea.** Iwapo una maswali, haujui jinsi ya kuendelea au unaamini mhusika wa tatu wa biashara anakiuka sheria za biashara wasiliana na Idara ya Maadili na Utekelezaji au Idara ya Sheria mara moja

### SWALI LA MAISHA HALISI

**S Mteja anayetarajiwa wa Hormel Foods yuko katika nchi iliyo chini ya vikwazo vya kiuchumi. Usafirishaji wa moja kwa moja kwa mteja huenda ukasababisha ucheleweshaji wakati wa kutafuta idhini ya ndani ya Kampuni na kungojea wakuu wa serikali waidhinishe usafirishaji huo. Je! tunaweza kusafirisha vifaa kwa mtu wa tatu katika nchi ambayo haitoi vikwazo hivi ili kuzuia kucheleweshwa?**

J La. Kusafirisha bidhaa kwenda mahali pa kati ili kuepukia sheria zinazosimamia bashara ya kimataifa ni marufuku. Wasiliana na Idara ya Sheria ya Hormel Foods kuzungumza juu ya wasiwasi wako au maswali. Kwa idhini sahihi –na kwa idhini sahihi tu – Hormel Foods yaweza kusaidia mteja katika nchi iliyo chini ya vikwazo vya kiuchumi vya Marekani.

# Kukataa Ufisadi na Hongo

Hapa Hormel Foods, tumejitolea kufanya kazi zetu kwa uaminifu na uadilifu, bila kutumia hongo au matendo mengine ya ufisadi. Kutoa au kupokea hongo au malipo mengine yasiyofaa kunakiuka sera zetu na sheria popote tunapofanya biashara. Ni muhimu kuzuia hata kuonekana kwa ushawishi kwenye maamuzi yetu ya biashara kutoka kwa malipo yasiyofaa au aina yoyote ya ufisadi.

## INAVYOMAANISHA

### Hongo

ni kitu chochote cha thamani ambacho hupewa kushawishi maamuzi ya mtu katika serikali au sekta binafsi ili kupata faida ya biashara, fedha, udhibiti au biashara. Hongo sio pesa taslimu kila wakati. Zawadi, huduma za kujitolea, safari, burudani au hata ofa ya kazi inaweza kutazamwa kama rushwa.

### Malipo ya uwezeshaji,

au "kiinua mgongo," kawaida ni kiwango kidogo cha pesa anayopewa afisa wa serikali wa ngazi ya chini ambayo inakusudiwa kuhamasisha au kuharakisha utendeji wa kawaida au hatua ya lazima ambayo ni sehemu ya kazi ya afisa huyo. Mifano ya vitendo hivi ni pamoja na huduma ya barua, kupata leseni au vibali, au kusindika hati za serikali kama visa. Sheria nyingi huchukulia haya kuwa malipo yaliyo katazwa, na yasiyofaa.

### Afisa wa serikali

ni mtu yeyote anayefanya kazi kwa au ni wakala wa chombo ambacho kinamilikiwa au kudhibitiwa na serikali. Hawa ni pamoja na maafisa waliochaguliwa na walioteuliwa katika ngazi yoyote ya serikali, na pia maafisa wa vyama vya kisiasa na wagombea wa ofisi. Maafisa wa serikali pia wanaweza kuwa watu binafsi katika ufalme, kama vile mwana wa mfalme.

# Tenda Linalofaa

- **Fuata sheria na sera zetu.** Sheria ya Desturi za Rushwa ya Kigeni ya Marekani (FCPA), Sheria ya Rushwa ya Uingereza na sheria kama hizo za ufisadi zinafikia ulimwengu na zinahusiana haswa na rushwa inayotolewa kwa wafanyikazi wa serikali au maafisa. Sheria hizi lazima zifuatwe wakati wowote. Usipatiane au kukubali hongo au malipo mengine ya aina yoyote yasiyo sawasawa.
- **Fuatilia wabia wa wahusika wengine.** Tunawajibika kwa matendo ya mhusika wa tatu yeyote ambaye anatuwakilisha, pamoja na mawakala, wasambazaji, washauri, na wapatanishi wengine na wawakilishi. Ikiwa utashirikisha mmoja wa wahusika hawa wa tatu, mfuatilie kwa uangalifu. Kuwa macho juu ya mtu yeyote anayefanya biashara kwa niaba ya Kampuni ambaye anaweza kujulikana kwa desturi za kibiashara zinazotiliwa shaka. Ikiwa ni muhimu kutumia mhusika wa tatu kama huyo, angalia kwa makini matendo ya mtu huyo au shirika hilo.
- **Hakikisha kuwa vitabu na rekodi ziko sahihi.** Hesabu za kweli na rekodi za fedha ni muhimu kuelezea wazi na kuhifadhi malipo ya aina yoyote.
- **Ongea kuhusu ufisadi.** Ripoti jambo hilo ikiwa malipo ya ewezeshaji au hongo imeombwa, iwapo utagundua mwenendo mwingine wowote ambao unaweza kuwa wa rushwa au una swali kuhusu uwezekano wa ufisadi. Wasiliana mara moja na msimamizi wako, Idara yetu ya Sheria au Afisa Mkuu wa Utekelezaji. Unaweza pia kuripoti bila kujulikana kwa nambari ya simu ya Maadili na Utekelezaji.



## SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Ninashughulika kupata kibali kilichoidhinishwa cha kujenga kituo kipya katika soko mpya kwa ajili ya Hormel Foods. Afisa wa vibali wa ndani amekuwa mwepesi sana katika kushughulikia ombi langu na amedokeza kila wakati ninapopiga simu kuwa pesa kidogo chini ya meza ingeongeza kasi ya kibali. Tunayo makataa ya kutimiza, na ninaogopa tutakosa malengo yetu ikiwa tutaendelea kungojea. Je, Naweza kumpa yeye malipo kidogo tu?**

**J** La. Hili sio suluhisho sahihi. Mara nyingi kupitisha suala hilo kwa mkubwa wa afisa kutatatua tatizo. Ikiwa sivyo, wasiliana na Idara yetu ya Sheria kujadili chaguo zingine.

NYENZO

### Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Sera ya Kupambana na Rushwa ya Shirika la Hormel Foods
- Taratibu za Ukaguzi wa Kina wa Washirika wa Tatu wa Shirika la Hormel Foods



PATA KUFAHAMU

## MIFANO YA SHUGHULI ZILIZOKATAZWA

- **Udanganyifu.** Kutoaminika au udanganyifu wa aina yoyote, kama vile malipo ya bonasi au nyongeza kwa washirika wa tatu kwa shughuli za kutiliwa shaka au zisizo wazi.
- **Kukwepa sheria.** Shughuli zinazokusudiwa kuegemea sheria zinazohusu uhifadhi, au malipo kwa, mawakala au washauri.
- **Kugushi.** Kurekodi maandishi yoyote ya uongo au bandia kwenye vitabu na rekodi za Kampuni.
- **Malipo ya Uwezeshaji.** Haya hayaruhusiwi katika nchi zingine ambazo tunafanya biashara. Kwa hivyo, sisi na washirika wetu hatuwezi kamwe kutoa malipo kama hayo kwa niaba ya Kampuni bila idhini ya maandishi kutoka kwa Afisa Mkuu wa Fedha, Wakili Mkuu au yule aliyemwacha.
- **Pesa taslimu kama malipo.** Malipo ya pesa taslimu na malipo, isipokuwa kwa kiwango kizuri kutoka kwa akaunti ndogo ndogo na zilizorekodiwa vizuri kwa mahitaji halali na ya kawaida ya biashara.
- **Hundi zinazolipwa kwa pesa taslimu au mmiliki.** Vighairi vitafanywa tu na idhini ya maandishi ya awali kutoka kwa Afisa Mkuu wa Fedha au anayeteuliwa.
- **Safari ambazo zimelipiwa gharama zote.** Malipo ya nauli ya ndege, makaazi, chakula na gharama zingine zinazohusiana na safari, zilizopatianwa au kukubalika.

# Kuzingatia Uwajibikaji wa Mazingira

Tumehamasishwa kucheza sehemu yetu katika kuzifanya jamii zetu na ulimwengu wetu kuwa bora kwa kuwa wasimamizi wazuri wa mazingira ya asili. Kujitolea kwetu kuhifadhi mali asili zetu kwa kupunguza uzalishaji wa gesi chafu, kuokoa maji na kupunguza matumizi ya nishati isiyoweza kulipwa na taka ngumu ni kipaumbele katika shughuli zetu popote tunapofanya biashara. Tunatarajia kujitolea kama hii kupanua katika ugavi wetu wote na kwa washirika wengine wa tatu wa biashara.

## Tenda Linalofaa

- **Dhamini mazingira.** Cheza sehemu yako kulinda mazingira ya asili na uyalinde kwa uangalifu. Fuata sheria zote zinazotumika za mazingira na sera za Kampuni ambazo zinatumika kwa kazi yako, popote tunapofanya biashara. Sisi wote tunafaa kucheza sehemu yetu ili kulinda ulimwengu wetu wa kiasili.
- **Chunguza hatari za kimazingira.** Hizi ni tabia hatari kama utupaji taka mbaya au kutolewa kwa vichafuzi, ambavyo lazima viripotiwe.
- **Hakikisha ripoti ni sahihi na kamili.** Hii ni muhimu haswa na michakato ambayo inaweza kuathiri mazingira, kama vile kupima, kurekodi au kuripoti kutokuwa na uzalishaji kwa mazingira, au kushughulikia takataka hatari.
- **Kuwa mwangalifu kwa desturi za wahusika wa tatu.** Fuatilia hatua yoyote ya mshirika wa biashara ambayo inaweza kukiuka viwango vya Kampuni kwa utunzaji wa mazingira. Washirika wa tatu ni ugani wa Kampuni yetu wanapofanya kazi kwa niaba ya Kampuni, kwa hivyo matendo yao lazima yalingane na viwango vyetu.
- **Ongea.** Ripoti tuhuma yoyote au maarifa kuhusu ukiukaji wa sheria na sera za mazingira katika shughuli zetu au katika shughuli za washirika wetu wa biashara, ukitumia njia yoyote ya kuripoti katika Kanuni hii.

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S Tuna mchakato wa uzalishaji ambao hutumia kontena mingi ndogo za kiungo mbichi ambazo haziwezi kuchakatwa tena. Kwa miaka mingi, nimeona idadi kubwa ya kontena hizi zikitupwa. Nilimwuliza msimamizi wangu ikiwa kiungo hiki kinaweza kupatikana katika makasha ya bidhaa nyingi, lakini akasema hakufikiria hivyo. Bado nina wasiwasi juu ya takataka zote. Je, kuna jambo zaidi naweza kufanya?**

J Kufuatilia suala hilo ni jambo sahihi kabisa. Ni wajibu wa kila mmoja wa memba wa timu kutafuta njia tunavyoweza kulinda mazingira vyema. Ufungaji wa malighafi unaweza kubadilika kwa muda, na vifurushi vingi vinaweza kupatikana sasa. Tafadhali wasiliana na Mkurugenzi wa Utunzaji wa Mazingira na wasiwasi wako ili suala la kontena lichunguzwe na kwa matumaini liboreshwe.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Ripoti ya Wajibu wa Shirika la Hormel Foods - Taarifa ya Sera ya Mazingira
- Sera ya Mazingira ya Hormel Foods
- Kanuni za Wajibu wa Wauzaji wa Hormel Foods
- Sera za Kilimo Endelevu za Hormel Foods



# Kutetea Haki za Kibinadamu

Sisi ni watetezi sugu wa haki za binadamu. Hormel Foods imejtolea kukuza na kulinda haki hizi za kimsingi ndani ya shughuli zetu na katika ugavi wetu. Unyanyasaji wowote wa haki za binadamu hautakubaliwa popote kwenye shirika letu au katika utendaji wa washirika wetu wa kibiashara.

## Tenda Linalofaa

- **Heshimu haki za binadamu.** Hii huanza na jinsi tunavyotendeana na washirika wetu wa kibiashara. Inajumuisha kufuata sheria zinazokataza kazi ya kulazimishwa na ya lazima, ajira kwa watoto, ubaguzi wa ajira na usafirishaji haramu wa binadamu. Fanya sehemu yako kukuza ujumuishaji na utofauti kwa kudumisha haki na kujiheshimu kwa kila mtu unayeshirikiana naye.
- **Fuatilia wabia wa wahusika wengine.** Kuwa macho kwa hatua yoyote ya mshirika wa biashara ambayo inaweza kukiuka viwango vya Kampuni vya ulinzi wa haki za binadamu. Washirika wa tatu ni ugani wa Kampuni yetu wanapofanya kazi kwa niaba ya Kampuni, kwa hivyo matendo yao lazima yalingane na viwango vyetu.
- **Ongea.** Ripoti tuhuma yoyote au ushahidi wa ukiukaji wa haki za binadamu, au ukiukaji wa sera na sheria zinazohusiana katika shughuli zetu au katika shughuli za washirika wetu wa biashara ukitumia njia yoyote ya kuripoti katika Kanuni hii.

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Nilimtembelea mmoja wa wauzaji wetu kufanya tathmini ya ubora. Nikiwa pale kiwandani, niliona wafanyikazi kadhaa ambao walionekana wachanga sana. Nilimwuliza muuzaji ikiwa walikuwa na umri wa kufanya kazi, lakini sikupata jibu wazi. Nifanye aje sasa?**

**J** Ulifanya jambo linalofaa kwa kuuliza muuzaji. Hata hivyo, jambo hilo bado linafaa kuchunguzwa. Unafaa kuripoti jambo kwa kuwasiliana na msimamizi wako au raslimali nyingine ya Kampuni. Ikiwa matumizi ya wafanyakazi walio umri wa chini imedhibitishwa, tutauliza muuzaji abadilishe mazoezi haya. Ikiwa hilo halijafanywa, tutakata uhusiano wa Kampuni na muuzaji.



NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Ripoti ya Uwajibikaji ya Shirika la Hormel Foods
- Sera ya Haki za Binadamu

# Kujiunga na Shughuli za Kisiasa

Tunaheshimu haki za memba wa timu kushiriki shughuli za kisiasa kuunga mkono vyama vya kisiasa, vikundi, wagombeaji au maafisa wa serikali. Unapojiunga na shughuli hizi, ni lazima iwe wazi kuwa unafanya kibinafsi na si kama mwakilishi wa kampuni.

## Tenda Linalofaa

- **Fuata sheria na sera za Kampuni.** Jukumu la Kampuni katika shughuli za kisiasa na ufadhili limezuiliwa na sheria na kanuni popote tunapofanya biashara. Timu yetu ya Masuala ya Kutunga Sheria inahakikisha sauti ya Kampuni inasikika katika maamuzi muhimu yaliyofanywa na maafisa wa serikali. Ushiriki wa Kampuni katika shughuli za kisiasa lazima uwe sahihi, ufuate sheria zinazotumika na uidhinishwe na Makamu wetu wa Rais wa Masuala ya Sheria.
- **Mali isiyohamishika na fedha za Kampuni.** Usiwahi tumia mali isiyohamishika au fedha za Kampuni kufanya michango ya kisiasa kwa niaba ya Kampuni.
- **Usijihusishe na ushawishi.** Hakuna mtu anayeruhusiwa kushiriki katika shughuli za utetezi wa kisiasa au kushawishi kwa niaba ya Kampuni. Masilahi ya Hormel Foods katika maswala ya sheria, udhibiti na sera huonyeshwa kwa wabunge kupitia Makamu wetu wa Rais wa Masuala ya Bunge na/au kamati teule ya hatua za kisiasa (PAC).
- **Ongea.** Ikiwa una maswali au wasiwasi juu ya shughuli za kisiasa au michango, wasiliana na raslimali iliyoorodheshwa kwa Kanuni hii kwa mwongozo.



### PATA KUFAHAMU

## JIWAKILISHE

Jiendeshe kwa hiari yako mwenyewe unapojiunga na shughuli za kisiasa. Hii hapa ndiyo jinsi ya kulifanya.

- **Usiwahi tumia muda wa kufanya kazi kwa shughuli zako za kisiasa.** Shughuli hizi lazima ziwe za hiari na zifanyike kwa wakati wako wa kibinafsi, kwa kutumia fedha za kibinafsi. Usiwahi omba michango ya kisiasa au usambaze machapisho wakati wa saa za kazi. Tunawahimiza memba wa timu kushiriki katika mchakato wa kidemokrasia na kupiga kura. Walakini, ikiwa huwezi kupiga kura wakati wa saa zisizo za kazi na unahitaji kupiga kura katika uchaguzi wakati wa kazi, wasiliana na msimamizi wako.
- **Ongea kama mtu binafsi.** Kuwa wazi kuwa maneno na maoni yako ya kisiasa ni yako pekee na si ya Kampuni.
- **Shiriki katika siasa kama raia binafsi.** Memba wa timu wanaruhusiwa kutoa michango ya kibinafsi kwa wagombea na vyama vya kisiasa vya hiari yao.

### SWALI LA MAISHA HALISI

**S Mgombea wa ofisi katika uchaguzi wa mitaa anauliza ikiwa angeweza kukodisha trela ya Hormel Foods kutoka kituo chetu ili kutumia kama uwanja wa hafla ya kampeni ya nje ya uchaguzi wake. Je, ninaweza kumuazima?**

J La, hauwezi. Michango ya kifedha au ya aina fulani au kitu kingine chochote kinachopewa mgombea wa kisiasa, hata ikiwa ni ya thamani ndogo, inaweza kuiweka Kampuni kwa sheria za kifedha za kampeni za serikali na majukumu ya kuripoti. Ombi lolote kutoka kwa mgombea wa kisiasa au afisa aliyechaguliwa kutumia mali ya Kampuni au fedha za kiwango chochote lazima liidhinishwe mapema na Makamu wa Rais wa mambo ya kutunga sheria.

# Kuhudumia Jamii Zetu

Tunaamini sana katika kuchangia wakati, talanta na hazina ili kusaidia jamii zetu za ulimwengu. Tunazingatia juhudi zetu za uhisani juu ya njaa, elimu na kusaidia maeneo tunayofanya biashara. Hormel Foods inatuhimiza sisi sote kuhusika na jamii zetu na kushiriki katika hafla zinazofadhiliwa na Kampuni zinazosaidia wengine.

## Tenda Linalofaa

- **Tuwakilishe kwa kujivunia.** Unapojitolea wakati wako au kutoa pesa kwa sababu ya jamii kama mwakilishi wa Kampuni, kuwa mweledi, mwenye adabu na mwenye heshima.
- **Chukua hatua za kibinafsi katika jamii yako.** Unaweza kukusanya haki za binadamu, ushiriki katika kuchakata hafla, kuchangia juhudi za kusaidia njaa na kujiunga na shughuli nyinginezo zinazosaidia jamii zenye nguvu. Hata hivyo, usiwahi kuwalazimisha wengine kushiriki au kuchangia misaada ya jamii unayopenda.
- **Usitoe michango ya hisani kwa niaba ya Hormel Foods.** Kuanzia pesa taslimu hadi michango ya bidhaa hadi udhamini, utoaji wa misaada hupangwa na Mawasiliano ya Shirika. Wasimamizi wa viwanda wana busara ya kutoa misaada ambayo haijapangwa katika kiwango cha shirika.
- **Kuwa mwangalifu kwa mizozo.** Hakikisha kuwa ushiriki wako wa kiraia, kama kushiriki katika bodi ya jamii ambayo inahitaji kujitolea masaa mengi ya wakati wako, haigongani na majukumu yako ya kazi au masilahi ya Kampuni.

## SWALI LA MAISHA HALISI

**S** **Binti yangu ni mshiriki wa programu ya vijana, na kila mwaka anapenda kuuza kuki kama njia ya kuchangisha pesa kwa ajili ya shirika hilo. Memba wa timu ninaofanya kazi nayo hukaa wakiulizia wakati raundi inayofuata ya mauzo ya vitafunio itaanza, kwa sababu wanataka kununua aina wanazopenda. Wakati vitafunio vile vinapatikana, je! Ninaweza kuacha karatasi ya kuagiza kwenye chumba cha kupumzika kwa wafanyikazi wenzangu?**

**J** Ndio, hilo ni sawa. Wachangishaji wa fedha kwa malengo kama vile mchango wa vitafunio wa vijana unaruhusiwa ikiwa hautamshinikiza mtu yeyote kununua vitafunio.

NYENZO

## Ili Kujifunza Mengi Zaidi

- Ripoti ya Uwajibikaji ya Shirika la Hormel Foods



# Muhtasari wa Nyenzo

Kanuni Zetu haziwezi kushughulikia kila hali unayoweza kukumbana nayo unapofanya kazi katika Hormel Foods. Ikiwa Kanuni haitoi mwongozo wa kutosha juu ya suala fulani na huna uhakika wa jambo sahihi la kufanya au kuwa na wasiwasi, wasiliana na msimamizi wako au raslimali hizi zingine zozote kwa usaidizi.

- Idara ya Maadili na Uzingatiaji – **EthicsandCompliance@hormel.com**
- Idara ya Kisheria – **LawDepartment@hormel.com**
- Idara ya Raslimali Watu (Marekani) – **HumanResources@hormel.com**
- Idara ya Raslimali Watu (Uchina) – **HumanResources@hormel.com.cn**
- Idara ya Raslimali Watu (Brazili)– **RecursosHumanos@ceratti.com.br**
- Idara ya Ukaguzi wa Ndani – **InternalAudit@hormel.com**
- Idara ya Mawasiliano ya Shirika – **Corporate_Communications@hormel.com**

## JINSI YA KUFIKIA NAMBARI YA DHARURA YA MAADILI NA UZINGATIAJI YA HORMEL FOODS

- Tumia tovuti hii bila kujitambulisha: **https://hormelfoods.ethicspoint.com.**
- Nchini Marekani na Kanada, piga simu ya Dharura ya Maadili na Uzingatiaji: 1-833-672-1232.
  - Inchini Uchina, piga: 400-120-0204.
  - Inchini Brazili, piga: 0800-000-0092.
  - Nje ya Marekani., Kanada, Uchina na Brazili, piga nambari yako ya ufikiaji wa nchi, ambayo inaweza kupatikana katika: **www.business.ATT.com/collateral/access.html.**
  - Unapopiga nambari yako ya ufikiaji wa nchi, utaulizwa nambari ya simu ya dharura ya Marekani. Kisha utaunganishwa kwa Mtaalamu wa Mawasiliano kwa lugha asilia.
- Simu zote zinaweza kupigwa bila kujitambulisha.
- Mawasiliano yote na ripoti zitashughulikiwa kwa usiri kadri iwezekanavyo.